SportPesa
TZS. 433,401,140
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Jina** la Sabaya laibua mvutano kisheria kortini

UKURASA 3




UKURASA 11

Jumatano Agosti 18, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580676

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## VIGOGO BANDARI WATIMULIWA NA BUNGE

UKURASA 2

# Askofu Gwajima matatani

**WAZIRI** aagiza polisi wamkamate, kisa...*Endelea ukurasa 2*



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima

Askofu Josephat Gwajima



UKURASA 3

Rais Samia Suluhu Hassan akihudhuria Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ulioanza jijini Lilongwe, nchini Malawi jana. Kushoto ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba. **PICHA NA IKULU**

# Samia aomba teknolojia ya utengenezaji chanjo corona

UKURASA WA 4

## PAROKO AFUTIWA SHTAKA KUMPA MTOTO UJAUZITO

PAROKO wa Parokia ya Manushi ya Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi, Padri Erasmus Swai (44), anayekabiliwa na kesi ya kumsababishia ujauzito mwanafunzi wa kidato cha...

UKURASA WA 7

## WALIOHUKUMIWA KUNYONGWA KWA KUMUUA MAMA WAFUTIWA ADHABU

MAHAKAMA ya Rufani Kanda ya Bukoba imewafutia adhabu ya kunyongwa hadi kufa watoto watatu waliotiwa hatiani kwa madai ya kumuua mama yao baada ya kumtuhumu kuwa...



UKURASA WA 2

## BASIL MRAMBA AFARIKI DUNIA

WAZIRI aliyedumu katika awamu nne za uongozi, Basil Mramba (81), amefariki dunia.

Mramba aliyekuwa waziri katika serikali ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, awamu ya pili ya Ali Hassan Mwinyi, awamu ya tatu ya Hayati Benjamin...

**MICHEZO** HABABUU AAHIDI MAKUBWA SIMBA QUEENS MICHUANO CAF UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Basil Mramba afariki dunia

**Na Romana Mallya**

WAZIRI aliyedumu katika awamu nne za uongozi, Basil Mramba (81), amefariki dunia.

Mramba aliyekuwa waziri katika serikali ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, awamu ya pili ya Ali Hassan Mwinyi, awamu ya tatu ya Hayati Benjamin Mkapa na ya awamu ya nne ya Jakaya Kikwete, alifariki dunia jana katika hospitali binafsi ya Regency jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na mtoto wake, Godfrey Mramba, baba yake alifariki dunia majira ya asubuhi.

Alisema wanafamilia wachache wataruhusiwa kufika kutoa pole nyumbani kwa marehemu barabara ya Mawenzi, Oysterbay, Dar es Salaam.

Mramba aliwahi kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara na baadaye mwaka 200-2005 aliiongoza Wizara ya Fedha.

Mbunge wa Jimbo la Rombo, (CCM), Prof. Adolf Mkenda, alisema Mramba amekuwa mbunge wa jimbo hilo kwa miaka 20, na kwamba aliitumia nafasi yake kuijenga na kuendeleza wilaya ya Rombo.

"Wana Rombo tutamkumbuka kwa mengi na hatutasahau mafanikio aliyotuletea. Aliwahi kuwa waziri wa wizara mbalimbali," alisema na kuongeza:

"Kati ya mambo ambayo atakumbukwa ni juhudi zake za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, akiwa Waziri wa Fedha, aliondoa kodi na tozo ambazo zilikuwa kero kwenye uchumi," alisema.

Mramba akiwa Waziri wa Fedha katika serikali ya Mkapa, ndiye aliyefuta kodi ya maendeleo, akisema haikuwa na tija kufuatia malalamiko ya wananchi wengi kwamba ukusanyaji wake ulikuwa ukiwasababishia usumbufu.

Mramba alikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara katika serikali ya awamu ya kwanza. Aliiongoza wizara hiyo pia katika serikali ya Mwinyi pamoja na Wizara ya Kazi hadi 1995.

Mwaka 2006, aliteuliwa na Kikwete kuwa Waziri wa Miundombinu, mwaka huo huo akahamishwa wizara na kupelekwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuanzia Oktoba 10, 2006 hadi mwaka 2008.

# Askofu Gwajima matatani

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amemtaka Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, kuthibitisha kauli yake kuhusu chanjo ya UVIKO-19 dhidi ya viongozi wa serikali, vinginevyo akamatwe.

Askofu Gwajima ambaye ni Mbunge wa Kawe (CCM), ametakiwa kuthibitisha shutuma alizozitoa hivi karibuni dhidi ya kuwapo kwa viongozi wa serikali kupokea hongo ili kuingiza chanjo ya UVIKO-19 nchini.

Dk. Dorothy alitoa agizo hilo jana wilayani Butiama mkoani Mara katika ziara yake ya kukagua hali ya utoaji huduma za afya na lishe pamoja na shughuli za maendeleo ya jamii.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya jana, ilibainisha kuwa endapo Askofu Gwajima atashindwa kuthibitisha hilo, vyombo vya dola vimchukulie hatua.

Waziri huyo alisema uongozi wa Hayati Dk. John Magufuli ulihimiza kujiridhisha na chanjo na uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan umejiridhisha kuwa chanjo ni salama, hivyo hajutii jitihada anazofanya.

"Sijutii kuhimiza matumizi ya tiba asili na sikubali upotoshaji juu ya alichosema Hayati John Magufuli kuhusu uingizaji chanjo.

"Hakuzuia chanjo zisiingie, pamoja na kutoa maagizo kuhusu usalama wa chanjo mwisho wa yote kwenye hotuba yake Chato Januari 27, mwaka huu alisema 'Wizara ya Afya isiwe inakimbilia chanjo bila yenyewe kujiridhisha', hivyo wizara imetekeleza wajibu wake," alisema.

Kauli ya waziri huyo imetoka ikiwa ni siku chache tangu Askofu Gwajima aendelee kutilia mkazo msimamo wake kuhusu kutokubaliana na chanjo ya UVIKO-19.

Mara kadhaa Askofu Gwajima amekuwa akiwaaminisha waumini wake kuwa chanjo hiyo sio salama, hivyo wasichanje.

Askofu Gwajima alianza kuonyesha kwenda kinyume cha msimamo wa serikali siku moja baada ya serikali kupokea awamu ya kwanza ya msaada wa dozi 1,058,400 za chanjo dhidi ya virusi vya corona.

Waziri wa Afya, Dk. Dorothy, ameendelea kuwahakikishia Watanzania kuwa chanjo hiyo ni salama kwa matumizi, hivyo wajitokeze kuendelea kuchanja.

Nipashe ilimtufuta Askofu Gwajima kwa njia ya simu kuzungumzia agizo la waziri huyo, lakini simu yake ilikuwa inaita pasi na kupokewa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe (kushoto), akizungumza na wafanyakazi wa kiwanda cha kusindika nyama cha SAAFI, mjini Sumbawanga, mkoani Rukwa juzi. **PICHA: IBRAHIM HAMIDU**

# Vigogo wa Bandari watimuliwa bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imewatimua vigogo wa Mamlaka ya Bandari (TPA) kikaoni na kuwapa wiki mbili kujipanga upya kujibu hoja za ukaguzi baada ya kamati hiyo kutoridhishwa na majibu waliyotoa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema TPA walipata hati isiyoridhisha katika ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutokana na mifumo yao kutokuwa mizuri.

"Mifumo haijakaa vizuri, tumewaambia Ofisi ya CAG watuletee taarifa za ukaguzi maalum uliofanyika ili kuwa na uamuzi sahihi.

"Bado inaonyesha hawa watu hawajafanya lolote, wanasuasua sana, hata wahasibu wao walionekana hawajui kazi maana hata maswali waliyoulizwa wameshindwa kujibu, tumewarudisha, warudi tena baada ya siku 14," alisema.

Alibainisha kuwa kamati hiyo imewahi kuagiza TPA kurekebisha mifumo yake kutokana na kutosomana na inatumika wa fedha.

"Hii mifumo inasababisha upotevu wa fedha kwa kuwa vitu vyao havipo wazi, wanajua mifumo ikitengenezwa vizuri itakuwa na uwazi mkubwa, tunajua kwamba bandari bado ipo kwenye asilimia 40 ya makusanyo ya fedha za mapato," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa bado kuna alichokiita madudu ndani ya TPA na hivyo kunatakiwa mifumo hiyo kusomana na kuwa wazi.

"Hata hoja za ripoti ya mwaka 2019/20, hazijafanyiwa kazi, bado kuna kusuasua. Kwa kuwa tulimwagiza CAG kufanya ukaguzi maalum na ndio walikuwa wanamalizia, tunasubiri atuletee ndani ya muda huo ili tusome pamoja na ripoti ya 2019/20," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, alisema Bunge lilitoa maagizo ya mifumo ambapo zaidi ya mwaka mmoja na nusu hayajatekelezwa hadi sasa.

"Imeonekana maagizo ya Bunge yamedharauliwa na hayajafanyiwa kazi na mifumo wanayoendelea nayo haina tija kwa taifa.

"Kwa hiyo, tunataka waje baada ya wiki mbili wakajipange waje na maelezo ya kutosha ya namna ya kuja na mfumo mzuri utakaokuwa na maslahi mapana ya taifa letu kwa kuzingatia umuhimu wa bandari katika nchi yetu," alisema.

CAG katika ripoti yake kwa mwaka 2019/20 aliyotoa mapema mwaka huu, aliibua vitendo vya ubadhirifu katika Bandari za Mwanza na Kigoma ambapo kwa Mwanza Sh. bilioni 3.7 zilitolewa kwenye akaunti ya TPA iliyoko CRDB kupitia miamala 737 huku vitabu vya fedha havikuonyesha hati za malipo na pia matumizi ya fedha hizo hayakuonyeshwa.

Katika Bandari ya Kigoma, Sh. milioni 655.9 zilitolewa kutoka benki kwa kutumia hundi 30 bila kuwa na hati ya malipo kuthibitisha malipo yaliyofanywa na hundi hazikusajiliwa kwenye daftari la udhibiti wa hundi, na vipande vitano vya hundi havijaonekana kwenye daftari la udhibiti wala taarifa za benki.

Vilevile, nyaraka kama vitabu vya hundi, hati za uhamishaji fedha na taarifa za bodi ya zabuni hazikutolewa kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Ripoti hiyo ilibainisha ukosefu wa ripoti za mapato za kila siku ili kuhakiki ripoti za mapato ya kila mwezi kwa kipindi cha miezi saba.

HABARI KITAIFA

## Mhitimu chuo kikuu aishtaki HESLB

**Na Thobias Mwanakatwe**

MHITIMU wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira Arusha, Alexanda Bakunguza, amefungua kesi Mahakama Kuu dhidi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akipinga elimu ya juu kugharamiwa na serikali kwa njia ya mikopo.

Katika kesi hiyo namba 16 ya mwaka 2021, mhitimu huyo anatetewa na mawakili watatu kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ambao ni Mpale Mpoki, Steven Mwakibolwa na Amani Jowachim.

Kesi hiyo iko chini ya majaji watatu wa Mahakama Kuu ambao ni Jaji Victoria Makani, Jaji Benihaj Masoud na Jaji Opiyo.

Mhitimu huyo anadai hoja yake ya msingi ni kwamba tozo na riba katika mikopo wanayopewa wanafunzi wa elimu ya juu inamchelewesha mwanafunzi kupata maendeleo japokuwa ameshaelimika.

Kufuatia hali hiyo, anadai elimu ya juu igharamiwe na serikali kuanzia mwanzo wa masomo hadi mwisho bila mwanafunzi kulipishwa gharama yoyote.

Msingi wa madai hayo unatokea kwenye Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inaeleza kuwa serikali itafanya jitihada kuhakikisha watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vinginevyo vya mafunzo.

Hata hivyo, kesi hiyo imewekewa mapingamizi matatu na serikali ikisema haina mashiko hivyo ifutwe.

Kesi hiyo ilifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza Julai 29, mwaka huu na jana ilitarajiwa kutolewa uamuzi juu ya mapingamizi yaliyowekwa na serikali.



Wapita njia wakivuka Barabara ya Morogoro, Mbezi Mwisho, mkoani Dar es Salaam jana, bila kutumia daraja la waenda kwa miguu, hali ambayo inaweza kuhatarisha usalama wao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia ataka teknolojia Afrika uzalishaji wa chanjo ya corona

**Na Mwandishi Wetu,** LILONGWE

RAIS Samia Suluhu Hassan ameziomba nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kushawishi kampuni zinazozalisha chanjo kuridhia vibali na teknolojia zao zitumike ili kuruhusu chanjo kuzalishwa katika nchi mbalimbali kukidhi mahitaji yaliyopo.

Samia alisema hayo jana mjini hapa alipokuwa akihutubia kwa mara ya kwanza Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC na kujitambulisha rasmi tangu aliposhika wadhifa huo Machi, mwaka huu. Pia alisema ni vyema nchi za SADC kushirikiana katika kubadilishana mbinu na uzoefu na kuwaelimisha wananchi kuhusu dhana potofu dhidi ya chanjo hizo pamoja na kuwahimiza kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na janga hilo. Sambamba na hilo, aliziomba nchi zilizoendelea na taasisi za kifedha za kimataifa kuendelea kutoa misamaha au kurefusha muda wa ulipaji wa madeni kwa nchi zinazoendelea mpaka pale janga hilo litakapokwisha.

Katika hotuba yake, Rais Samia alisema Malawi ni taifa la kwanza katika nchi za SADC kuongozwa na Rais mwanamke, hivyo kujitambulisha kwake katika mkutano huo kutaongeza msukumo kwa wanawake wengi zaidi kujiamini na kuhamasika kushiriki kwenye vyombo vya uamuzi.

Alisema viongozi wa SADC hawana budi kushirikiana katika kuendeleza jitihada za kuwainua na kuwawezesha wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi na uamuzi katika nchi zao.

Pia aliwafahamisha viongozi wa SADC kuwa katika mkutano wa 'Generation Equality' uliofanyika hivi karibuni nchini Ufaransa, alichaguliwa kuwa kinara wa Masuala ya Haki za Kiuchumi za Wanawake, hivyo kuomba ushirikiano kutoka kwao ili yeye na timu yake watekeleze jukumu hilo kikamilifu. Alisema katika kipindi cha miaka 40 tangu kuanzishwa kwa SADC kumekuwa na mafanikio na changamoto mbalimbali, hivyo akiwa kiongozi mpya katika jumuiya hiyo, ameahidi kutoa ushirikiano ili kusukuma ajenda za utengamano, kushughulikia changamoto na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo.

Rais Samia alimpongeza Rais wa Malawi, Dk. Lazarus Chakwera, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa SADC na kumpongeza Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, kwa kazi kubwa na nzuri ya kuiongoza jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Vilevile, Rais Samia alimpongeza Katibu Mtendaji wa SADC anayemaliza muda wake, Dk. Stagomena Tax, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye jumuiya hiyo kwa kipindi cha uongozi wake na kuiwakilisha vyema Tanzania katika jumuiya hiyo.

# Jina la Sabaya laibua mvutano wa kisheria

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MVUTANO wa kisheria umeibuka mahakamani katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, baada ya Upande wa Jamhuri kuomba mahakama kufanya marekebisho madogo kwenye hati ya mashtaka na kuweka jina la Sabaya badala ya Sayaba.

Mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha jana, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula, aliomba mahakama hiyo, kuruhusu Upande wa Jamhuri kufanya marekebisho madogo ya jina la tatu ili lisomeke Sabaya badala ya Sayaba kwenye hati ya mashtaka.

Kesi hiyo ya jinai namba 105 ya mwaka huu inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo, Sabaya na wenzake wawili wakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Wakili Chavula alidai jina la mshtakiwa lipo sahihi katika maeneo mengi kwenye hati hiyo isipokuwa katika maelezo ya mashtaka yote matatu limekosewa kutokana na makosa ya uchapaji na kusomeka Sayaba badala ya Sabaya.

Hata hivyo, Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alipinga ombi hilo na kuomba mahakama hiyo kulikataa sababu limekuja wakati mshtakiwa ameshatoa utetezi wake.

"Hati hii ndio iliyomkuta na kesi ya kujibu na mshtakiwa amejitetea kwa maelezo haya haya na amemaliza na Upande wa Jamhuri ukafunga kesi yao baada ya kuleta mashahidi 11, sasa leo kuomba marekebisho haiwezekani, wamechelewa," alidai.

Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, aliiomba mahakama kuwasikiliza na kuwaruhusu ili wafanye marekebisho hayo madogo ambayo alidai yanaruhusiwa kisheria.

Hakimu Amworo aliahirisha kesi hiyo kwa muda ili kutoa uamuzi mdogo na baadaye waliporejea, alisema mahakama inaruhusu marekebisho hayo ya jina la mshtakiwa wa kwanza.

"Maombi ya marekebisho madogo hayatakiuka haki ya mshtakiwa wa kwanza hivyo yanakubaliwa," alisema.

Hakimu huyo alisema wakili wa mshtakiwa wa kwanza anapewa mwongozo wa nafasi ya mwongozo kutoa ushahidi wake wa msingi tena kuhusu jambo hilo.

Baada ya uamuzi huo kutolewa, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Chavula, aliwasomea upya mashtaka yao washtakiwa wote watatu kwenye maelezo ya makosa matatu yaliyokosewa jina hilo kwenye hati ya mashtaka.

Washtakiwa wengine mbali na Ole Sabaya ni Sylvester Nyegu na Daniel Mbura ambao wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha na wote walikana.

Baada ya kusomewa hati hiyo, Wakili wa Utetezi, Mahuna, alimwongoza mshtakiwa wa kwanza, Ole Sabya, juu ya jina lake kutajwa katika mashtaka hayo.

Sabaya alidai anashangaa jina lake kutajwa kwa kuhusishwa na mashtaka hayo ambayo hajahusika nayo.


IN THE HIGH COURT OF TANZANIA (COMMERCIAL DIVISION)

AT DARES SALAAM COMMERCIAL CASE NO. 99 OF 2020

CRDB BANK PLC ..............................................................PLAINTIFF

VERSUS

MAIGE EZEKIEL MAGOLYO ..........................................DEFENDANT

DECREE

**WHEREFORE;** The Plaintiff prays for judgment and decree against the Defendant as follows: -

a) Payment of the principal sum of Tanzania Shillings One Hundred Eighty Four Million Six Hundred Eighty Three Thousand Eight Hundred Eighty Seven and Twenty Two Cents (i.e. TZS., 184,683,887.22), all accruing interest at 18°/o and penalties at 3% from 24 September 2020 to the date of full payment.
b) Payment of Commercial interest at 21°/o per annum on (a) above from 30th August, 2020 to the date of full payment.
c) Payment of General damages to the tune of Tanzania Shillings One Hundred Million (i.e. TZS 100,000,000.00).
d) Payment of interest on decretal sum at the rate of 12°/o.
e) Costs of this suit.
f) Any other relief(s) as the court may deem fit and just.

This matter coming for Judgment on this 10th day of August, 2021 before Hon K. T. R. Mteule, Judge in the presence of Advocate Catherine Tibasana for the plaintiff and in absence of the Defendant.

THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT;

a) Payment of the principal sum of Tanzania Shillings One Hundred Eighty Four Million Six Hundred Eighty Three Thousand Eight Hundred Eighty Seven and Cents Twenty Two (TZS 184,683,887.22), all accruing interest at 18°/o and penalties at 3°/o from 24 September 2020 to the date of full payment.
b) Payment of Commercial interest at 21°/o per annum on (a) above from 30th August, 2020 to the date of full payment.
c) Payment of General damages to the tune of Tanzania Shillings One Hundred Million (TZS 100,000,000.00).
d) Payment of interest on decretal sum at the rate of 12°/o. e) Costs of this suit.

Given under my hand and seal of the court on this 10th day of August 2021.




216412902

# Samia atoa bil. 300/- kukamilisha ujenzi mji wa Serikali wa Mtumba

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa kikosi kazi cha taifa cha kuratibu serikali kuhamia Dodoma na ujenzi wa mji wa serikali Mtumba, Meshack Bandawe, amekutana na wakurugenzi wa utawala na rasilimali watu wa wizara zote kujadili maandalizi na utekelezaji wa ujenzi wa ofisi za ghorofa za wizara zitakazojengwa awamu ya pili katika mji huo.

Kikao hicho kinafuatia maelekezo ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliyezitaka wizara kuanza taratibu za ujenzi wa ofisi za awamu ya pili baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa Sh. bilioni 300 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu na majengo ya ghorofa yatakayotumiwa na wizara mbalimbali katika mji wa serikali Mtumba.

"Kwakuwa wakurugenzi wa utawala na rasilimali watu wa wizara ndiyo timu ya ufundi ya usimamizi wa ujenzi na wasaidizi wa makatibu wakuu ni vyema tukajipanga kikamilifu ili kutekeleza ujenzi kwa tija, ufanisi, ubora, muda, kanuni, taratibu na kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa na serikali," alisema Bandawe.

Kwa mujibu wa Bandawe, kikao hicho pia ni maandalizi ya vikao vitakavyofuata vya makatibu wakuu na mawaziri kwa ajili ya kupokea maagizo na maelekezo ya serikali katika kutekeleza shughuli za ujenzi kwa ufanisi. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa mji wa serikali ilikamilika Aprili, 2019 na kuwezesha wizara na taasisi mbalimbali za serikali kuhamishia ofisi zake mkoani Dodoma na ujenzi wa awamu ya pili ya mji huo unatarajiwa kuanza muda wowote kuanzai sasa baada ya serikali kutoa pesa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo.



Katibu wa kikosi kazi cha taifa cha kuratibu serikali kuhamia Dodoma na ujenzi wa mji wa Serikali Mtumba, Meshack Bandawe, akiongoza kikao cha wakurugenzi wa utawala na rasilimali watu wa wizara zote. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani aomba kaburi liondolewe shuleni

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

DIWANI wa Chibe Manispaa ya Shinyanga, Peter Kisandu, amelalamikia kuwapo na kaburi katikati ya Shule ya Msingi ya Mwalugoye ambalo limekuwapo kwa zaidi ya miaka 17.

Kisandu alibainisha hayo jana kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani Manispaa ya Shinyanga wakati akiuliza maswali ya papo kwa papo.

Alisema katika shule hiyo iliyopo Chibe Manispaa ya Shinyanga, kuna kaburi katikati ya shule hiyo, ambalo linahitajika kuondolewa ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri.

"Mkurugenzi nauliza swali, ni lini serikali itafanya uthamini wa kuondoa kaburi ambalo lipo katikati ya Shule ya Msingi Mwalugoye," aliuliza Kisandu.

"Eneo la ujenzi wa shule hiyo lilitolewa na wananchi na kulikuwa na kaburi la mwenye mji na serikali ikasema italifanyia tathmini na kuliondoa, lakini mpaka sasa miaka 17 bado lipo," aliongeza.

Katika hatua nyingine diwani wa Kizumbi, Lubeni Kitinya, naye aliuliza swali juu ya hatima ya kufanyia marekebisho ubovu wa taa za barabarani, ambazo haziwaki na kuufanya mji huo kuwa giza.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, akijibu maswali hayo, alisema suala la kuondoa kaburi katika ya shule hiyo litafanyiwa kazi kwa kukutana na ndugu wa familia na kufanya nao tathmini.

Alisema suala la matengenezo ya taa za barabarani lipo chini ya mkandarasi, serikali imeshazungumza naye na hivi karibuni atazifunga upya.

# Paroko afutiwa shtaka kumpa mtoto ujauzito

**Na Godfrey Mushi,** HAI

PAROKO wa Parokia ya Manushi ya Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi, Padri Erasmus Swai (44), anayekabiliwa na kesi ya kumsababishia ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne, amefutiwa shtaka hilo katika Mahakama ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

Kwa sasa Padri Swai anakabiliwa na shtaka moja la kumbaka mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 17 (jina limehifadhiwa), ambaye alikuwa akisoma Shule ya Sekondari Kimaseki iliyoko mkoani Arusha.

"Mahakamani leo (jana), Jamhuri wameondoa shtaka la kumpa mimba mwanafunzi, wamebaki na shtaka la ubakaji na wameomba muda ili wamalize upelelezi wao na tutakuja kwa ajili ya kutaja kesi hiyo Septemba 16 mwaka huu," alidai Wakili wa Utetezi, Monica Mushi.

Kwa mujibu wa wakili huyo, Padri Swai sasa atakabiliwa na shtaka la kubaka ambalo kesi yake itatajwa tena mahakamani huko Septemba 16, mwaka huu.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi wa Wilaya hiyo, Thurston Kombe, Upande wa Mashtaka ukiwakilishwa na Mwendesha Mashtaka, Philbert Mashurano.

Kabla ya kufutiwa kosa la kumpa ujauzito mwanafunzi huyo, padri huyo alikuwa akidaiwa kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 60 (A) (3), Sura ya 353 cha Sheria ya Elimu.

Awali katika hati ya mashtaka, Padri Swai alidaiwa kutenda makosa hayo Machi mwaka jana, akiwa katika Hoteli ya Snow View iliyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa mshtakiwa alitenda kosa la kwanza la kubaka chini ya kifungu cha 130 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Penal Code), Sura 16 ya Sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

**"Mahakamani leo (jana), Jamhuri wameondoa shtaka la kumpa mimba mwanafunzi, wamebaki na shtaka la ubakaji na wameomba muda ili wamalize upelelezi wao na tutakuja kwa ajili ya kutaja kesi hiyo Septemba 16 mwaka huu," alidai Wakili wa Utetezi, Monica Mushi.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Migogoro ya wakulima, wafugaji ifikie kikomo*

**MAPIGANO** kati ya wakulima na wafugaji, kwenye baadhi ya maeneo nchini, ni miongoni mwa migogoro ambayo imekuwa ikiibuka kama uyoga na kutafutiwa ufumbuzi na mamlaka husika, lakini imeendelea na kuwa tishio kwa usalama.

Kuna matukio mengi ambayo ni mifano ya migogoro hiyo ambayo imetokea miaka ya nyuma na kusababisha maafa, vikiwamo vifo na uharibifu wa mali kwa makundi hayo mawili na jamii kwa ujumla. Tukio la juzi la mapigano kati ya makundi hayo wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro ni mfano unaoonyesha jinsi migogoro ya ardhi ilivyo tatizo kubwa na tishio kwa amani. Diwani wa Masama Rundugai wilayani humo, Aziz Simbano na wenzake wawili akiwamo na mwanawe wa kiume, walinusurika kuuawa, baada ya kujeruhiwa na wafugaji waliotaka kulisha kwa nguvu mifugo katika mazao yake. Migogoro kama hiyo imekuwa ikitokea mara kadhaa katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Pwani, Manyara, ingawa serikali ilijaribu kufanya jitihada za kuitatua.

Moja ya hatua ni kuundwa kwa tume iliyoongozwa na Profesa Issa Shivji mapema miaka ya 2000, baada ya kutokea mgogoro mkubwa wa ardhi wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro, uliosababisha vifo na uharibifu mkubwa wa mali. Moja ya mapendekezo ya tume hiyo ilikuwa kutengwa kwa ardhi kwa ajili ya matumizi ya malisho ya mifugo na kilimo.

Katika baadhi ya maeneo kwa mfano, wilayani Mvomero mkoani Morogoro, serikali ilitekeleza pendekezo hilo, ingawa kwa maeneo mengi hilo halijafanyika. Lakini kwa tukio hilo la wilayani Hai, tunadhani kwamba ipo haja kwa serikali kuongeza jitihada za kumaliza kabisa migogoro kati ya wakulima na wafugaji, ambayo kwa sasa ni tishio la amani na usalama wa nchi.

Njia mojawapo ambayo tunadhani inaweza kusaidia kupunguza migogoro, ni kutengwa kwa maeneo ya malisho na kuyatambua kisheria ili kuzuia uvamizi unaoweza kufanywa na watumiaji wengine wa ardhi. Wakiwa na maeneo yao yenye malisho na maji ya kutosha wakati wote, ambayo yanatambuliwa kisheria, tunaamini hawatahama ovyo na kujikuta wakigombana na wakulima kutokana na tuhuma za kulisha mazao yao.

Kwa miaka mingi Watanzania wamekuwa wakiishi mchanganyiko kuanzia wakulima na jamii ya wafugaji, huku wafugaji wakitumia ufugaji wa asili na kuchangia katika ukuaji wa soko la nyama.

Hata hivyo, utamaduni wa kuhama kila wakati kutafuta maji na malisho, umekuwa ukidaiwa kuchangia kuwapo kwa migogoro kati yao na wakulima, huku wakulima nao wakituhumiwa kujeruhi mifugo na wakati mwingine kudaiwa kuikamata.

Kwa mazingira kama hayo, tunadhani umefika wakati sasa tofauti za makundi hayo kumalizwa, ili yaishi kwa amani kutokana na ukweli kwamba yote yanategemeana kwa namna moja au nyingine.

Mfugaji anaweza kununua mazao kutoka kwa mkulima, na pia mkulima anaweza kununua mfugo au kitoweo kutoka kwa mfugaji, hivyo tunaamini ushirikiano wa makundi hayo ni wa muhimu kuliko utengano.

Wote ni Watanzania, wana haki ya kutumia ardhi kulingana na taratibu zilizowekwa, ndio maana tunashauri kutafutwa kwa njia ya kudumu ambayo inaweza kumaliza uhasama huo wa miaka nenda rudi.

Hatukubaliani kwa namna yoyote na migogoro hiyo kwa sababu imekuwa ikisababisha upotevu wa maisha ya watu na uharibifu wa mali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Neema Sawaka

# *Kwandikwa wewe ni taa iliyozimika ghafla*

**AGOSTI 2** mwaka huu, mshumaa ulizima ghafla pale alipoondoka duniani, Elias Kwandikwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Ushetu -CCM, baada ya kuishi duniani miaka 55.

Kwandikwa mwana- Ushetu jimbo lililoko mkoani Shinyanga, watu

mbalimbali wanakulilia kutokana na matendo mema uliyoyafanya hapa duniani, wanasema wapigakura wako.

Mmoja wa wanaohuzunika zaidi ni Meneja wa Wakala wa Barabara wa Taifa (TANROADS), mkoani Shinyanga, Mibara Ndirimbi, anayesema

marehemu Kwandikwa atakumbukwa kwa maono yake ya kuleta maendeleo wakati alipokuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuongeza mtandao wa barabara kwa kiwango cha changarawe na lami.

Ndirimbi anasema Kwandikwa alifanya jitihada kuweka taa za barabarani na kujenga kilomita nne za lami kwenye makao makuu ya Halmashauri ya Ushetu yaliyopo Nyamilangano.

Anasema Kwandikwa katika siku za uhai wake, alishiriki kufungua barabara mbalimbali na alizozindua ni ile ya Bugomba A, kwenda Ulowa mpaka Bulungwa yenye kilomita 22 kwa kiwango cha changarawe na Muhuridede-Tulole kwenda mkoani Tabora yenye urefu wa kilomita 21 kwa kiwango cha changarawe.

"Kupitia juhudi zake mradi wa taa za barabarani uligharimu zaidi ya Sh. milioni 200 na barabara alizoziunganisha zimeweza kuleta mawasiliano bora na kurahisisha usafiri na usafishaji wa mizigo na mazao. Haya ndiyo aliyoyafanya Kwandikwa katika uhai wake. Ni mshumaa tulioutaka uendelee kuwaka," anasema Ndirimbi. Meneja wa TANROADS anamkumbuka akisema Hayati Kwandikwa siku za maisha yake alikuwa mshauri mkubwa wa miradi ya barabara na aliongeza mtandao wa barabara hasa katika Jimbo la Ushetu kwa kuunganisha barabara za Mikoa ya Mwanza na Tabora, Katavi na Geita.

Diwani wa kata ya Sabasabini, Emanuel Makashi, anamtaja Hayati Kwandikwa kuwa ni mtu wa kipekee siyo kwenye familia yake tu, hata kwenye jamii na aliweza kuunganisha barabara ambazo tangu uhuru zilikuwa hazipitiki baada ya kuteuliwa na Hayati John Magufuli kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

Wakazi wa Ushetu, Juma Manyanda na Cecilia Mihambo wanasema kuwa mbunge wao aliendelea kujitoa kwa kuwajengea madaraja makubwa ya Kidanha North Upper , Bulugwa, Kasheshe Lower na South Bulungwa.

Manyanda anasema madaraja ya Karo, Ulewe pamoja na Mgaya hayakujengwa tangu uhuru na kazi hiyo ya kutukukuka imewaondolea kero wananchi na tatizo la mifugo kufa kwa kusombwa na maji.

"Kujitoa kutusaidia kwa juhudi zake na kufa kwake ni pengo. Wengi wameathirika sana pamoja na kuwa ni mipango ya Mungu bado wataendelea kumkumbuka"anasema Manyanda.

Cecilia anapomkumbuka Kwandikwa anasema vikundi vya wanawake kupitia kwake, viliungana na kujenga umoja, ili kuanzisha shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

Anasema waziri na mbunge wao alisisitiza wanawake ambao hawajajiunga wajiunge na waliokuwa kwenye vikundi aliwasaidia mawazo na maono ambayo yaliwasaidia wengi kupitia vikundi vyao.

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Nyamilangano, Makoye Juma anasema mchango wa mawazo ya Hayati Kwandikwa vilikuwa nuru na msukumo wa maendeleo kwa wananchi wa wote wa Ushetu.

Makoye anaeleza kumfahamu Kwandikwa kabla ya hajawa mbunge na alikuwa akipenda watu na kutaka maendeleo.

Hayati Kwandikwa alizaliwa mwaka 1966 na katika uhai wake alisoma na kufanya kazi katika nafasi mbalimbali serikalini zikiwamo za kisiasa kama mbunge wa Ushetu, Naibu Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

## Mahakama Tanzania yapata mtendaji mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, kuwa mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilisema Prof. Ole Gabriel anachukua nafasi ya Mathias Kabunduguru ambaye amestaafu utumishi kwa mujibu wa sheria.

Aidha taarifa hiyo ilisema Prof. Ole Gabriel ataapishwa Agosti 21 pamoja na mabalozi wateule waliopangiwa vituo vya kazi ambao ni Luteni Jenerali Yakub Hassan Mohamed (Uturuki), Mahmoud Thabit Kombo (Italia) na Elsie Sia Kanza (Marekani).

Katika hatua nyingine Rais Samia amemteua Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU).

## Wajasiriamali 100 kumiliki viwanda

**Na Romana Mallya**

ZAIDI ya wajasiriamali 100 wanatarajia kumiliki viwanda vidogo vya kubangua korosho kupitia mpango maalum wa kuongeza ubanguaji wa zao hilo unaosimamiwa na kampuni ya Kamal.

Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Gagan Gupta, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na wajasiriamali hao ambao alisema kwa sasa wanapitia katika programu maalumu wanayoiendesha kabla ya kukabidhiwa viwanda hivyo vitakavyojengwa eneo la viwanda Zinga, Bagamoyo.

"Huu ni mwendelezo wa mradi huu tuliouzindua mwezi Januari mwaka huu, mpaka sasa tumewapata wajasiriamali zaidi ya 100. Bado tunaendelea kuwakaribisha wengine wenye nia ya kumiliki viwanda vya kubangua korosho," alisema.

Alisema mjasiriamali atahitaji kuwa na Sh. milioni 16.92 ambazo zitakuwa sawa na asilimia 20 ya jumla ya kiasi cha Sh. milioni 84.6 zinazohitajika kuendesha kiwanda cha kubangua korosho.

"Kiasi kinachobakia cha Sh. milioni 67.68 ambacho ni sawa na asilimia 80 ya mahitaji kitapatikana kwa kupitia mkopo kutoka benki itakayoshirikiana na Kamal katika kudhamini mradi.

# Waliohukumiwa kunyongwa kwa kumuua mama wafutiwa adhabu

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Kanda ya Bukoba imewafutia adhabu ya kunyongwa hadi kufa watoto watatu waliotiwa hatiani kwa madai ya kumuua mama yao baada ya kumtuhumu kuwa ni mchawi.

Uamuzi huo ulitolewa mbele ya jopo la majaji watatu ambao ni Jacob Mwambegele, Rehema Kirefu na Panterine Kente baada ya kupitia sababu za kukata rufani na hoja za Jamhuri.

Rufani hiyo iliwasilishwa na Alex Minani, Emmanuel Minani na Issaya Simon, dhidi ya Jamhuri wakipinga hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu Biharamulo.

Walalamikaji wanadaiwa Machi 29, 2013 muda wa saa mbili usiku maeneo ya Karamba, Kijiji cha Muhimila wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, walimuua mama yao Gaudencia Simon.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi watano na vielelezo viwili ikiwamo ripoti ya uchunguzi ya daktari, huku walalamikaji wakijitetea wenyewe bila kuwa na mashahidi.

Shahidi wa kwanza wa Jamhuri ambaye ni mke wa mlalamikaji namba tatu, alidai siku ya tukio marehemu akiwa na mtoto wake Nahimana Issaya, mjukuu wake Furaha Issaya na mwanaye ambaye ni mlalamikaji namba tatu Simon, alitembelewa na watoto wake wawili.

Alidai aliingia mlalamikaji namba moja Alex na Emmanuel na mlalamikaji wa kwanza alimtuhumu mama yake kuwa anamroga mkewe, lakini marehemu alikana tuhuma hizo.

Shahidi huyo wa kwanza alidai walalamikaji wote walianza kumpiga mama yao kwa kutumia fimbo za mihogo kuanzia saa mbili usiku hadi saa nne usiku.

Alidai marehemu alipiga kelele, lakini mlalamikaji namba moja alimziba mdomo baada ya muda alikwenda mke wa mlalamikaji namba mbili akamchukua mume wake na kuondoka naye nyumbani.

Shahidi alidai mlalamikaji namba moja aliendelea kumpiga hadi kusababisha kifo chake, alichukua mwili na kwenda kuutupa mtoni na alimuonya asitoe siri hiyo.

Ilidaiwa baada ya kuripotiwa polisi tukio hilo, waliutafuta mwili na kuukuta msituni, katika ripoti ya uchunguzi ilionyesha sababu ya kifo ni kukosa hewa.

Walalamikaji katika utetezi wao walikana kuhusika katika tukio hilo na kuongeza kwamba siku ya tukio walikuwa nyumbani wamelala na wake zao. Mahakama baada ya kusikiliza ushahidi huo iliwatia hatiani washtakiwa na kuwahukumu kunyongwa hadi kufa.

Walalamikaji walipinga adhabu hiyo wakiwa na sababu 11 ikiwamo kwamba Jaji wa Mahakama Kuu alikosea kuwatia hatiani na kuwahukumu kunyongwa kwa kuzingatia ushahidi wa shahidi namba moja. Walidai ushahidi wa shahidi huyo haueleweki na mahakama haikupaswa kuuamini.

Upande wa Jamhuri ulidai ushahidi wa shahidi wa kwanza ulijitosheleza kwa kuwa alielezea tukio zima na alishuhudia tukio. Rai yao upande wa mashtaka kuwa walithibitisha makosa bila kuacha shaka, waliomba rufani itupwe.

Jopo la majaji baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili ilikubaliana na sababu ya kwanza kwamba ushahidi wa shahidi namba moja ambaye ni mke wa mlalamikaji namba tatu haueleweki.

"Baada ya kuondoa ushahidi wa shahidi wa kwanza hakuna ushahidi mwingine unaoonyesha washtakiwa walitenda kosa.

"Kama Jaji wa Mahakama Kuu aliondoa katika kumbukumbu, shahidi wa kwanza asingefikia uamuzi wa kuwatia hatiani washtakiwa na kuwapa adhabu ya kunyongwa," lilisema jopo hilo.

Mahakama ilikubaliana na sababu hiyo ya kwanza ya rufani, iliamua kufuta kutiwa hatiani na adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Iliamuru walalamikaji waachiwe huru gerezani kama hakuna makosa mengine ya kuwafanya waendelee kuwapo.



Madiwani wa Manispaa ya Shinyanga, wakipitia makabrasha kwenye kikao cha baraza cha kawaida jana, wakijadili ajenda mbalimbali, ikiwamo miundombinu ya barabara, elimu, maji, na umeme. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kortini kwa tuhuma za wizi mil. 75/-

**Hellen Mwango na Hadija Kitwana**

MTUNZA Fedha wa Bank of Afrika (BOA), Mahami Mwaipyana, amesomewa mashtaka saba ikiwamo wizi wa Sh. milioni 75 mali ya mwajiri wake akiwa mtumishi.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, alidai kuwa Januari 4, 2018 akiwa mtumishi wa benki ya BOA tawi la Mbezi Luis aliiba Dola za Kimarekani 8,200 kupitia nafasi yake ya utumishi.

Shtaka la pili, Novemba 29,2017 mshtakiwa anadaiwa kuiba Dola za Kimarekani 10,000 kupitia nafasi yake ya utumishi.

Katuga alidai kuwa shtaka la tatu na nne, kati ya Oktoba 18 na Machi 6, 2018 aliiba Dola za Kimarekani 17,700 kupitia nafasi yake ya utumishi.

Katika shtaka la tano mpaka la saba, kati ya Agosti 21, Novemba 16 na Agosti 18, 2017 mshtakiwa aliiba Sh. milioni 2.9 kupitia nafasi yake ya utumishi.

Mshtakiwa alikana mashtaka yote.

Katuga alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe fupi kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Pia alidai kuwa upande wa Jamhuri hauna pingamizi la dhamana dhidi ya mshtakiwa.

Hakimu Simba alisema, mshtakiwa awe na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 36 mmoja awasilishe atoe fedha taslimu Sh. milioni 36 au hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo.

Hata hivyo, hakimu alisema kesi hiyo itatajwa leo ili kumpa nafasi mshtakiwa kupeleka wadhamini na Agosti 24, mwaka huu, atasomewa maelezo ya awali.

Awali, upande wa Jamhuri uliomba kubadilisha hati ya mashtaka kutoka uhujumu uchumi na kutakatisha fedha na kuwa kesi ya jinai.

Hakimu alikubali ombi la Jamhuri na mshtakiwa alisomewa mashtaka hayo saba ya wizi akiwa mtumishi.

# Serikali yashusha gharama urasimishaji makazi

**Na Munir Shemweta, DODOMA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametangaza kupunguzwa gharama za urasimishaji makazi holela kutoka Sh. 150,000 hadi 130,000.

Licha ya kushusha gharama hizo, amesema kila mmiliki wa ardhi anayeishi mjini sasa lazima awe na hati.

Lukuvi alisema jana kuwa wananchi wasio na uwezo wa fedha kwa ajili ya urasimishaji, sasa watakopeshwa na Benki ya NMB ambayo imeingia makubaliano na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kazi hiyo.

Alisema si suala la hiari mmiliki wa ardhi kuwa na hati bali ni lazima na kubainisha kuwa katika kipindi cha miezi mitatu, taratibu za kutambua maeneo ya urasimishaji zifanyike ili kuanza urasimishaji huo.

Urasimishaji makazi holela umeanzishwa kwa ajili ya kutambua maeneo yaliyojengwa holela bila kufuata taratibu za mipango miji na ulianza mwaka 2013 na kutarajiwa kukamilika 2023.

Awali, katika urasmishaji huo, wananchi walitakiwa kulipia kwa viwango tofauti kuanzia Sh. 350,000 hadi 250,000 na baadaye Waziri Lukuvi alipunguza hadi kufikia Sh. 150,000.

Akizungumza na kampuni za upangaji, upimaji na watendaji wa sekta ya ardhi mkoani Dodoma jana, Lukuvi alisema, kazi hiyo ni ya lazima na kila mwananchi mwenye nyumba au kiwanja anayeishi mjini lazima awe amemilikishwa na kupatiwa hati.

"Uhamasishaji lazima ufanyike ili wananchi wajue kama wanapaswa kuingia katika urasimishaji na kuelewa umuhimu wa upatikanaji miundombinu, mfumo wa ukusanyaji na utumiaji fedha za urasimishaji makazi holela katika maeneo mbalimbali haukuwa mzuri na kwa kiasi kikubwa umekwamisha zoezi kwenda kwa kasi," alisema. "Tumekwama muda mrefu katika urasimishaji na sasa tumekubaliana na Benki ya NMB iwakopeshe na kulipa kwa riba ya asilimia 10," alisema Lukuvi.

Pia waziri aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri za wilaya kuanza kutambua na kuainisha kampuni zitakazofanya kazi za urasimishaji kwa kuangalia uwezo wa kila kampuni na kuunda kamati ya urasimishaji ya mtaa na kuanza zoezi.

"Mtakaoenda kufanya kazi lazima mfanye tathmini ya kazi au miradi iliyofanyika kwenye maeneo yenu ili kuona kazi zilizofanyika na zile zilizoshindwa kufanyika," alisema Lukuvi.

Pia alisema baada ya kukamilika zoezi la utambuzi, Benki ya NMB itatoa mkopo wa Sh. 130,000 na katika fedha hizo kampuni itapewa Sh. 120,000 huku Sh. 6,000 ikienda halmashauri kwa ajili ya miundombinu ya barabara na nyingine ikibaki kwa halmashauri kwa ajili ya taratibu za hati.



Wananchi wakiwa wamemdhibiti mtu mmoja kwa kumlaza chini, baada ya kutuhumiwa kumnyanyasa kijinsia mwanamke aliyekuwa akipita njia, eneo la Posta Mpya, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Idriss Sultan, wenzake waachiwa huru

**Hellen Mwango na Hadija Kitwana**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemwachia huru mchekeshaji Idriss Sultan (27) na wenzake baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), kuomba kuiondoa kesi hiyo kwamba hana nia ya kuendelea na kesi iliyokuwa inawakabili, dhidi ya kurusha maudhui mtandaoni bila kuwa na leseni.

Kesi hiyo imefutwa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Yusto Rubologa.

Wakili wa Serikali Neema Mushi, alidai kuwa DPP amewasilisha hati ya Nole chini ya kifungu cha 91 kidogo cha (1).

"DPP amewasilisha Nole kwamba hana nia ya kuendelea na kesi hii chini ya Kifungu cha 91 kidogo cha (1), ameomba kuiondoa kesi hii mahakamani na hana nia ya kuendelea nayo," alidai Mushi.

Hakimu Rubologa alisema, mahakama yake inakubali ombi la Jamhuri inawaachia washtakiwa huru chini ya kifungu hicho.

Mbali na Idriss, washtakiwa wengine ni, Doctor Ulimwengu (28) na Isihaka Mwinyimvua(22).

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Baltilda Mushi, ulidai washtakiwa hao walitenda kosa hilo kati ya Machi 8, mwaka 2016 na Machi 12, 2020 mahali tofauti jijini Dar es Salaam.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Batilda Mushi, alidai washtakiwa hao, walirusha maudhui online tv kwenye akaunti ijulikanayo Loko Motion bila kuwa na leseni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA).

Washtakiwa walikana shtaka hilo na walikuwa nje kwa dhamana.

## Bima afya kwa vikundi, familia

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imezindua huduma za mpya ijulikanayo 'Bima ya Afya na Maisha' ikilenga kuwezesha ushirikishwaji wa jamii katika kupata huduma za bima jamii kupitia familia na vikundi vya kijamii.

Miongoni mwa wanufaika wa bima hiyo ni vikundi vya vicoba, saccos, wafanyakazi, vikundi vya whatsApp na vyama vya ushirika.

Huduma hiyo inayopewa amana na Kampuni ya Bima ya Sanlam Life Insurance Tanzania inahusisha Bima ya 'Afya Salama' mahususi kwa ajili ya wana familia pamoja na Bima ya 'Nia Njema' ambayo ni mahususi kwa ajili ya wana vikundi mbalimbali vya kijamii pamoja na familia zao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Bima, Benki ya NBC, Benjamin Nkaka, alisema huduma hizo zinalenga kusaidia nia ya serikali katika kuhakikisha kwamba huduma ya bima ya afya inamfikia kila Mtanzania.

"Kupitia huduma ya Bima ya Nia Njema tunalenga kuwalinda Watanzania katika vikundi vyao vya kijamii na kiuchumi na wakati huo huo kuwezesha ushirikishwaji wa jamii katika mifumo ya fedha kwa kupitia bima za jamii ikiwamo vikundi vya vicoba, saccos, wafanyakazi, vikundi vya wafanyakazi, wajasiriamali, taasisi, vyama vya ushirika, makundi ya WhatsApp, na vikundi vingine vya namna hiyo," alisema.

Alifafanua kuwa bima ya vikundi inahusisha idadi ya wanachama kuanzia watano na kuendelea, ambao wanaweza kuwa wanandugu, wanamtaa au muunganiko wowote, huku akibainisha kuwa gharama ya kujiunga kwa mwaka ni Sh. 18,000.

"Utofauti wa bima hii ni kutoa huduma ya bima ya maisha kwa wanakikundi pamoja na familia zao, kwa gharama nafuu, uharaka na kwa utaalamu wa bima za jamii."

"Huduma hizi zinapatikana katika mikoa yote nchini na mafao ya bima hutolewa ndani ya saa 24 hadi 48, baada ya kuwasilisha taarifa na viambatanisho sahihi kutoka kwa uongozi wa kikundi na kujaza fomu ya madai. Utaratibu wa kujisajili ni kupitia kikundi," aliongeza.

Kuhusu Bima ya Afya Salama, Nkaka alisema inalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kiafya kwa wana familia na inatumika katika hospitali zaidi ya 372 kote nchini ikiwamo hospitali za serikali na hospitali binafsi.

Mkuu wa Idara ya Bima kupitia benki kutoka Kampuni ya Sanlam, Klispinana Shirima, aliwahakikishia wateja wa huduma hizo kuwa ni bora na zinalenga kuwagusa wanajamii moja kwa moja, huku akibainisha kuwa kampuni hiyo imejipanga kuhakikisha huduma hiyo inatolewa kwa kukidhi matakwa na malengo ya kuanzishwa kwake.

# Ajali gari, pikipiki yaua na kujeruhi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Manispaa ya Lindi, mkoani Lindi, Juma Mmongo, amefariki dunia na mwingine kulazwa hospitalini baada ya pikipiki waliyokuwa wakisafiria kugongana na gari ndogo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Foka Dinya, alieleza ajali hiyo ilitokea juzi usiku katika eneo la Mitwero Barabara Kuu ya Kibiti- Lindi.

Alisema Mmongo aliyekuwa anaendesha pikipiki yenye namba MC 466 PQU, huku akiwa amembeba abiria, Masamaki Lugendigwa.

Alieleza kuwa pikipiki hiyo iligongana na gari ndogo aina ya Hiace yenye namba T. 830 PKQ ikiendeshwa na Said Selemani Daudi, mkazi wa Barabara ya Kawawa mjini hapa.

Alisema Masamaki Ndugendigwa, mfanyabiashara wa samaki, alijeruhiwa na amelazwa Hospitali ya Mkoa wa Lindi, Sokoine, na kwamba chanzo cha ajali hiyo ni uzembe uliotokana na dereva wa bodaboda kulipita gari lililokuwa mbele yake eneo lenye kona, ndipo ikagongana na gari hiyo.

# Elimu yatakiwa kwa walimu wanaoshushwa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MDHIBITI Mkuu Ubora wa Shule Kanda ya Mashariki, Victor Mbwindike, ameishauri serikali kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa walimu wa sekondari wanaoshushwa kufundisha shule za msingi ili wajitambue na kuziba mapengo ya upungufu wa walimu.

Alisema hayo wakati akizungumza na maofisa elimu wa kata mkoani Morogoro kwenye mkutano mkuu wa Umoja wa Maofisa elimu kata Tanzania (UMEKTA) mkoa.

Mbwindike alisema ipo haja kwa serikali kutoa elimu fupi kwa walimu hao ili kuziba mapengo ya upungufu wa walimu shuleni humo kufuatia malalamiko ya wakuu wa shule na maofisa elimu kata kuwa walimu wengi wakifika huko hawajui nini wanafanya.

Aidha, Mbwindike aliwataka waanzilishi wa shule za msingi na sekondari kuhakikisha wanafuata vigezo vinavyotakiwa kukamilishwa katika usajili wa shule kabla hawajaanza kulalamika kucheleweshwa katika suala la usajili.

Alisema wapo waanzilishi ambao wanataka kuanzisha shule bila kuhakikisha vigezo vinakamilika.

# Ruvuma ilivyozalisha ziada mahindi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKOA wa Ruvuma kwa mwaka 2020/2021 umezalisha ziada ya mahindi tani 326,497 kati ya tani za mahindi 816,242 zilizozalishwa.

Akizungumza wakati anazindua soko la ununuzi wa mahindi Kanda ya Songea mkoani Ruvuma katika Kijiji cha Mgazini Halmashauri ya Songea, Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alisema katika kipindi cha mwaka 2020/2021, wakulima wa mahindi wamelima hekta 276,488.

"Uzalishaji huu ni zaidi ya kiwango kilichozalishwa kwa ongezeko la asilimia nne, ikilinganishwa na kiwango cha uzalishaji katika msimu wa mwaka 2019/2020 ambapo tani 787,321 pekee zilizalishwa," alisisitiza Ibuge.

Brigedia Jenerali Ibuge alisema mkoa una uwezo wa kuuza ziada hiyo ndani na nje ya nchi ambapo aliupongeza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa uamuzi wa kununua mahindi ambayo ni sehemu ya ziada.

Alisema katika awamu ya kwanza ya ununuzi kutakuwa na vituo tisa katika mkoa mzima, ambavyo vimepangwa, kwa lengo la kumrahisishia mkulima kuuza mahindi yake bila kutumia gharama kubwa.

Hata hivyo, alisema kiwango cha kununua tani 32,000 tu za mahindi kwa Mkoa wa Ruvuma ambacho kimewekwa na NFRA ni kidogo ikilinganishwa na uzalishaji mkubwa wa mahindi uliofanywa na wakulima msimu huu.

Alisema mgao huo ni kidogo, hivyo alitoa rai kwa Wizara ya Kilimo kupitia NFRA kuendelea kushirikiana kupanua wigo wa masoko ili wakulima wa Ruvuma waendelee kuzalisha ziada.

Meneja wa NFRA Kanda ya Songea, Ramadhani Nondo, alisema kwa ujumla NFRA katika msimu wa mwaka 2020/2021, inatarajia kununua tani za mahindi 165,000 ambapo Kanda ya Songea imetengewa kununua tani 32,000, na kwamba kwa awamu ya kwanza zinanunuliwa tani 6,000.

Amesema mahindi yatanunuliwa kwa shilingi 500 kwa kilo katika kituo cha NFRA Ruhuwiko na vituo vingine yatanunuliwa kwa shilingi 470, na kwamba ununuzi utafanyika kwenye vituo tisa vilivyopangwa ambavyo ni Namtumbo Mjini, Namabengo, Mgazini, Magagura, Mpitimbi, Mbinga Mjini, Kigonsera na Ofisi za Kanda za NFRA Ruhuwiko.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge (kushoto), akikata utepe kuzindua soko la ununuzi wa zao la mahindi Kanda ya Songea, uliofanyika kimkoa katika kijiji cha Mgazini juzi. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# Diallo aibua mazito kwa RC Gabriel

**Na Mwandishi Wetu,** MAGU

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) MKoa wa Mwanza, Anthony Diallo, amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, kuhakikisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inachunguza ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Langi uliogharimu Sh. milioni 51.

Alitoa agizo hilo katika ziara ya kamati ya siasa ya mkoa huo wilayani Magu kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

Diallo alisema mradi huo unahitaji ukaguzi maalum ili kuona kama fedha zilizotumika katika ujenzi huo zinaendana na thamani halisi.

Miradi mingine iliyotiliwa shaka na Diallo ni wa maji unaosimamiwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) wilyani Magu.

Kwa mujibu wa Diallo, awali mradi huo ulikuwa unafanya kazi vizuri, lakini baada ya kukabidhiwa RUWASA umekuwa kero na kuomba ukabidhiwe kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira mkoani Mwanza (MWAUWASA).

Akizungumzia ukaguzi wa mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, alisema ulianza mwaka 2010, lakini na viongozi wengine waliokuwapo hawapo sasa.

Alimwomba Gabriel kukagua mradi huo kwani hawajui unaendeleaje kwa lengo la kutoa maelekezo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Sh. milioni 11 zinatarajiwa kuchangwa na wananchi ili kuendeleza ujenzi huo.

Awali Ofisa Mtendaj wa Kata ya Lutale, Emanuel Kasmiry, alisema ujenzi huo unahitaji Sh. milioni 62 hadi kukamilisha na zilizotumika mpaka sasa Sh. milioni 52.

Alisema wananchi walishirikishwa kuchangia mradi huo pamoja na fedha za halmashauri.

Alisema baada ya kukabidhiwa RUWASA ulianza kuwa na kero na kuomba ukabidhiwe kwa MWAUWASA

Katika ukaguzi wa mradi wa Shule ya Sekondari Nyasato Kata ya Jingimili alibaini kero ya umeme katika kijiji hicho ambayo imedumu kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Gabriel alimwagiza Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme (TANESCO), Mkoa wa Mwanza, Ibrahim Msafiri, kuandaa mpango ili kujua maendeleo ya mradi huo.

# Madini yazua mgogoro wilaya 2

**Na Thobias Mwanakatwe**

KUGUNDULIKA kwa madini aina ya Silicon katika kitongoji cha Kwebamba kumezua mvutano wa mpaka kwa wananchi wa Wilaya za Lushoto na Korongwe ambapo kila wilaya inadai kiko ndani ya wilaya yake.

Kutokana na mvutano huo, hali ya amani imeanza kuvunjika kufuatia baadhi ya wakazi wa Korogwe kuanza kuwatisha maisha wananchi kwa mapanga pindi wanapowakuta kwenye mashamba yao ambayo wamegawiwa na serikali ya kijiji.

Diwani wa Milingano, Peter Leonard, alisema kata yake ina vitongoji 22, ikiwemo kitongoji cha Kwebamba na kwamba aligombea akiwa anakitambua kitongoji cha Kwebamba kuwa kiko ndani ya Halmashauri ya Bumbuli wilaya ya Lushoto.

"Tunashangaa kuzuka kwa mgogoro huu wa kimpaka wakati inaeleweka wazi ramani ya eneo la kitongoji cha Kwebamba ambalo sasa limeingia kwenye mgogoro kati ya pande hizo mbili, imechorwa tangu kipindi cha mkoloni," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Bumba, Afizai Daffa, alisema serikali ya kijiji hicho ilianza utaratibu wa kugawa maeneo ya wazi kwa wananchi mwaka jana kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo.

Alisema wananchi wa Kwebamba kuendesha shughuli za kilimo kumekuwa na changamoto kutokana na kutishiwa maisha na kikundi cha watu kutoka wilaya ya Korogwe wakiambiwa ni wavamizi jambo ambalo linatishia kuvunjika kwa amani katika kitongoji hicho.

Naye aliyekuwa diwani wa kata hiyo kwa zaidi ya miaka 15, Hozza Mandia, alisema ramani inaonyesha kuwa kitongoji cha Kwebamba kiko eneo la Bumbuli.

Mandia aliwataka viongozi wa Korogwe kukaa meza moja na viongozi wa Bumbuli ili kumaliza mgogoro huo alioueleza kukosa sura nzuri kwa jamii.

Mandia alisema Halmashauri ya Bumbuli kupitia Mbunge, Januari Makamba, kwa kutambua kuwa kitongoji hicho kipo ndani ya jimbo hilo ambapo miradi kadhaa imetekelezwa.

Miradi hiyo ni pamoja na kuweka mabomba ya maji, mabati, saruji pamoja na shilingi milioni 5 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa shule .

Nao wananchi wa kitongoji cha Kwebamba wamemuomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kuingilia kati mgogoro huo wa ardhi.

Kwa mujibu wa wananchi, umiliki wa eneo hilo katika kitongoji cha Kwebamba na Msitu wa Bumba Mavumbi ambalo nalo limegunduliwa madini unaozigonganisha HalmashaurI Bumbuli na kijiji chao.

Mzee Athumani Akida (85) ambaye ni mwanzilishi wa kitongoji hicho, alisema hata wataalam kutoka ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 2009 walifika katika kitongoji hicho na kupima eneo hilo na kuweka mawe ya mipaka 'bikoni' yanayoonyesha kuwa eneo liko Bumbuli, Wilaya ya Lushoto.

Mkazi mwingine wa Kwebamba, Yohana Mwavu (73) naye alieleza kushangaa madai ya viongozi wa Korogwe na kusema kama kitongoji hichi kiko kwao kwa nini hakiwapatii huduma zozote za kijamii.

Mzee Mwavu alieleza kwamba huduma zote ambazo hivi wanazipata zinatoka Halmashauri ya Bumbuli.

Mkuu wa Wilaya Lushoto, Ekalist Lazalo, akizungumza na gazeti hili kwa simu alithibitisha kufahamu mgogoro huo na kwamba anajipanga kufika eneo hilo ili kujionea tatizo na kuwasikiliza wananchi.

Alisema baada ya kujionea tatizo atalazimika kukutana na Mkuu wa Wilaya ya Korogwe ili waone namna ya kutafuta suluhu ya mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi, alisema hana taarifa ya mgogoro huo, na kwamba endapo atapata taarifa ya mgogoro huo ataandika barua kwa Mkuu wa Wilaya ya Lushoto ili waangalie namna ya kutatua.




Mbunge wa Rufiji ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mohamed Mchengerwa, akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 83 kwa Meneja wa Maendeleo ya Jamii na Uchumi wa kampuni ya Songas, Nicodemus Chipakapaka (wapili kulia ), wakati wa hafla ya makabidhiano kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vyumba saba vya madarasa katika vijiji vya Shela na Kiwanga Rufiji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bil. 1/- yakarabati maktaba saba za mikoa

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imefanya ukarabati mkubwa wa maktaba saba za mikoa kwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 1.15.

Hatua hiyo ni mikakati yake ya kuleta mapinduzi kwenye sekta ya elimu.

Aidha, imejipanga kuhakikisha huduma hiyo inafika ngazi ya wilaya.

Akizindua jana maktaba ya Mkoa wa Iringa ambayo ilikuwa ikifanyiwa ukarabati, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema serikali imedhamiria kuboresha ubora wa elimu nchini.

Alibainisha kuwa Bodi ya Huduma ya Maktaba nchini ilikuwa na kero nyingi ambapo katika mwaka wa fedha ulioisha zilitengwa Sh. bilioni 1.15.

"Tukaamua kuanzia ofisi za mikoa saba na Iringa ni mojawapo ambapo walihitaji Sh.milioni 200 lakini tulifanikiwa kuleta Sh.milioni 150 kwa ajili ya kukarabati maktaba kabla ya ukarabati hali haikuwa nzuri," alisema.

Aidha, aliwataka watumishi wa maktaba nchini kuongeza ubunifu katika utendaji kazi wao na kurejesha utamaduni wa zamani wa Watanzania kujisomea.

"Nawaomba mwongeze ubunifu maktaba hizi zimejengwa siku nyingi wenzetu wa zamani waliona mbali lakini sisi wa kizazi hiki tumeanza kupoteza utamadini wa zamani, ningependa tuurudishe umuhimu wa kusoma fanyeni kazi kwa bidii tupo kwa pamoja," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Maktaba Taifa, Mboni Ruzegela, alishukuru wizara kwa kutoa fedha hizo za ukarabati wa maktaba nchini.

Alizitaja maktaba zilizofanyiwa ukarabati ni za Mikoa ya Iringa, Bukoba, Rukwa Kilimanjaro, Tabora, Kigoma na Morogoro.

Hata hivyo, alisema Mpango wa Mkakati wa Bodi ya Maktaba nchini ni pamoja na kushughulikia ramani za majengo katika sehemu ambazo hakuna huduma za maktaba.

Pia alisema wamepanga kutumia Sh. bilioni mbili kwa ajili ya maktaba mtandao 43 na 22 za mikoa na 19 ni za wilaya.

# Warundi waenda jela kisa kuishi nchini kinyemela

**Na Hadija Kitwana**

WATU sita raia wa Burundi wamehukumiwa kifungo cha miezi sita jela au faini ya Sh. milioni moja baada ya kukutwa na hatia ya kuingia nchini bila kibali.

Washtakiwa hao wamekwenda jela baada ya kushindwa kulipa faini.

Hukumu hiyo ilitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba baada ya washtakiwa kukiri mashtaka yao.

Mwendesha Mashtaka wa Idara ya Uhamiaji, Sitta Shija, alidai kuwa washtakiwa hao ni Said Bitingimana (25), Jafari Daudi (22), Uwimana Elia (23), Sendega Noel (21), Jafari Nderea (20) na Bikurumana Emmanuel (20), wote wakazi wa Chanika ambao ni raia wa Burundi.

Shija aliendelea kudai kuwa katika shtaka la kwanza linawakabili washtakiwa hao, Agosti 13, mwaka huu huko maeneo ya Chanika Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam wakiwa raia wa Burundi, waliingia Tanzania bila kuwa na hati ya kusafiria au nyaraka yoyote inayowaruhusu kuingia nchini.

Katika shtaka la pili, alidai kuwa washtakiwa wanakabiliwa na shtaka la kuwapo nchini bila kibali ambapo tarehe hiyo hiyo na eneo hilohilo walikuwa wakiishi nchini bila kuwa na viza au nyaraka yoyote inayowaruhusu kuishi.

Baada ya upande wa mashtaka kumaliza kusoma mashtaka hayo, washtakiwa wote walikiri kutenda makosa hayo na kuiomba mahakama kupunguziwa adhabu.

Hakimu Simba alisema kuwa kutokana washtakiwa kukiri makosa yao, anawahukumu kulipa faini ya Sh. milioni moja au kifungo cha miezi sita jela na baada ya kumaliza kifungo warudishwe nchini kwao Burundi.



Ukurasa 12

**AFGHANISTAN KAMA VIETNAM...**
Rais akimbia, Al Shabaab Somalia washereheka



Ukurasa 13

**Ruto anavyojipanga 'kutoboa' urais bila muungano kisiasa**


# siasa

JUMATANO AGOSTI 18, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

**Mhanga wa uhaini 'aliyempiga' rungu kwa kishindo Rais Lungu**

MKUTANO RAIS NA VYAMA

# Viongozi wa vyama vya siasa wanapotajiwa mbinu kufanikiwa

**Na Sabato Kasika**

MAPEMA mwaka huu katika hotuba yake bungeni, Rais Samia Suluhu Hassan ameahidi kukutana na vyama vya siasa, ili kuweka mwelekeo wa kuendesha shughuli za kisiasa zenye tija na masilahi kwa taifa.

Rais anasema, katika awamu ya sita amedhamiria kuendelea kulinda misingi ya demokrasia, uhuru wa watu na vyombo vya habari kwa kuwa masuala hayo ni msingi wa amani katika nchi na husaidia kuchochea maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Wakati Rais akipanga kukutana na vyama vya siasa, Aprili mwaka huu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, anakaririwa na vyombo vya habari akisema amemwandikia barua kumuomba akutane na chama hicho kutafuta ufumbuzi utakaoliletea taifa furaha, haki na ustawi.

Katika hilo, Mbowe anaeleza kuwa kauli ya Rais ya kutaka kukutana na vyama vya siasa, imegusa wengi wenye hofu ya Mungu ikiwamo CHADEMA. Hata hivyo msimamo wa kutaka kukutana na Rais wenyewe badala ya vyama vyote vya siasa, unaangalia na wadau kwa jicho la ziada.

**TUMUACHIE RAIS AAMUE**

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo Addo Shaibu, akizungumzia mkutano huo, anasema njia yoyote ambayo Rais ataamua kuitumia kwa lengo la kukutana na vyama vya siasa, chama chao kinaona ni sahihi.

"Siwezi kuzungumzia CHADEMA, ila ninachojua, Rais ameahidi kukutana na vyama vya siasa, iwe ni kukialika chama kimoja kimoja au vyote pamoja ama kutumia Kituo cha Demokrasia Tanzania, huo ni uamuzi wake," anasema Shaibu.

Aidha, anaongeza kuwa ACT-Wazalendo kimeshatoa ujumbe wao kupitia kwa Kiongozi Mkuu wa Chama Zitto Kabwe , wa kuomba Rais Samia akutane na vyama vya siasa, na kwamba wanazingatia ombi hilo na huo ndiyo msimamo wao kwa sasa na kuongeza kuwa pamoja na hayo, ingependeza iwapo Ikulu itakutana na vyama hivyo, ili mambo mbalimbali muhimu kwa ajili ya manufaa ya Tanzania na watu wake yajadiliwe.

**WASISAHAU CCM IMO**

Mchambuzi wa siasa Gwandumi Mwakatobe, anasema, anachojua ni ahadi ya Rais kukutana na vyama vya siasa ikiwamo CCM, siyo upinzani pekee kama ambavyo baadhi ya wanasiasa wanavyotafsiri, vinavyotajwa 'vyama vya siasa.'

"Nakumbuka, mara tu baada ya Rais Samia kuapishwa, CHADEMA walidai kuwa wameamuandikia barua ya kuomba kuonana naye, lakini akiwa bungeni, aliahidi kukutana na vyama vya siasa," anasema Mwakatobe na kukumbusha kuwa CHADEMA iliwahi kusema imejibiwa ombi lake la kutaka kukutana na Rais, ingawa majibu waliyopewa hayafahamu.

"Katika hotuba yake hivi karibu Rais anasema anaona vyama vya siasa vimenyumbulikanyumbulika, hali inayoonyesha kuwa nia yake ni kukutana navyo," anasema Mwakatobe na kuongeza kuwa vinapotajwa vyama hivyo CCM imo na kwamba anachotaka ni kukutana navyo vyote bila kujali ni vya upinzani au CCM ili kusikiliza changamoto na kubadilishana mawazo.



Nancy Mrikaria. **PICHA: MTANDAO**

"Kukutana na vyama vya siasa haina maana kwamba vitakosa fursa ya kueleza kero au matatizo yanayovikabili, bali ni nafasi ya pekee ambayo kila chama kinaweza kuitumia kufikisha ujumbe sehemu husika," anasema.

**KUJIAMINI ZAIDI**

Mkuu wa Idara ya Uhamasishaji, Kampeni na Uchaguzi ya Chama cha TLP, Nancy Mrikaia, anasema CHADEMA, kuandika barua na kutaka kukutana na Rais bila kushirikisha wengine ni kujiamini kulikopitiliza kuwa ndicho chama kikuu cha upinzani na hakuna kingine chenye sifa hiyo, viongozi wakidaiwa kujiona kama chama kina nguvu wakati sivyo.

Mwanasiasa huyo anaongeza kuwa tatizo jingine ni kujiinua na kuona vyama vingine havina umuhimu wakati vyote vinaunganishwa na kapu moja ya upinzani ambalo vyama vyenye usajili wa kudumu vinahusika.

"Ni vyema wasubiri ratiba ya Rais ya kukutana na wote, ndiyo maana vyama vingine vinaendelea kusubiri, kwani ahadi yake ni kukutana navyo, siyo CHADEMA kwanza," anaeleza na kukumbusha umuhimu wa umoja na kwamba haoni ni kwa nini upinzani utengane wakati unakazi moja.

Mjumbe wa Jukwaa la Katiba, Hebron Mwakagenda, anasema vyoyote atakavyoamua Rais kuhusu lengo lake la kukutana na vyama vya siasa ni sawa, kwa kuwa haoni tatizo.

"Matatizo ya vyama vya siasa yanatofautiana, kwani vipo ambavyo vina wabunge na madiwani, vina matatizo yake na vingine havina wabunge wala madiwani, navyo pia vina yake, "anasema Makagenda.

Anafafanua kuwa Rais anaweza kuamua kukutana na kila chama, ili kujua matatizo yanayokisibu na kisha kukutana na vyote kwa pamoja, au akaviweka katika makundi na kukutana navyo. Hivyo, haoni tatizo CHADEMA kutaka kukutana na Rais bila vyama vingine.

**TAIFA KWANZA**

Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia Dar es Salaam Abbas Mwalimu na mchambuzi wa siasa, anasema, mara nyingi vyama vinaongozwa na falsafa na itikadi hali inayosababisha vitofautiane. Lakini, yapo baadhi ya maeneo ambayo vinakubalina, hivyo ni muhimu vitangulize maslahi ya taifa kuliko ya vyama.

Anasema, kwenye suala la kukutana na Rais analiona katika taswira mbili ambazo ni falsafa na itikadi, pia ubinafsi wa baadhi ya vyama wa kudhani vyenyewe ndivyo vyenye haki kuliko vingine.

Anafafanua kuwa, katika utatuzi

**INAENDELEA UK.14**

# Afghanistan kama Vietnam...

• Rais akimbia, Al Shabaab Somalia washereheka, huenda Nigeria itafuata



Majeshi ya Taliban yakiongeza ulinzi mitaani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

HARAKATI za jihadi katika nchi nyingi za Kiislamu zimepata nguvu mpya baada ya ushindi wa kimbunga wa vikundi vya wapiganaji wa Taliban ambao sasa wanadhibiti Afghanistan na kumlazimisha Rais Ashraf Ghani, aliyekuwa anaungwa mkono na Marekani kuikimbia nchi.

Ni takriban siku 10 tangu kukamilisha utekelezaji wa amri ya Rais Joe Biden wa Marekani ya kuharakisha, kuondolewa vikosi vya nchi hiyo nchini humo, hatua ya mwisho au ya kuainisha kukamilika kwa zoezi hilo ilikuwa ni kukabidhiwa kambi ya jeshi la anga ya Bagram iliyoko karibu na Jiji la Kabul, mji mkuu wa Afghanistan.

Baada ya Waamerika kuondoka, waasi wa Taliban walianza kuteka miji midogo, halafu mikubwa na mwisho wamechukua nchi.

Kilichotokea Kabul ni marudio ya kuondoka kwa wanajeshi wa Marekani jijini Saigon nchini Vietnam Kusini mwaka 1975 na kundi kubwa la watu likipigania kuondoka pamoja nao.

Marekani kwa miaka 10 ilipigana na majeshi ya ukombozi wa chi hiyo, kuzuia utawala wa Kikomunisti wa Vietnam ya Kaskini, usiiteke nchi yote.

Vita hiyo iliyopamba moto wakati wa Rais Lyndon Johnson na Marekani ikiaondoka Vietnam muhula wa pili wa Richard Nixon.

Marekani ilipoamua kuharakisha kuondoa majeshi yake Afghanistan, kilichofuata ni kuondolewa uwezo wa serikali iliyokuwapo Ikulu kuendelea kudhibiti miji midogo na mikubwa, vivuko na njia za mawasiliano kote nchini humo, ili kudhibiti nyendo za wapiganaji wa Taliban.

Alichosema Rais Biden akitetea maamuzi yake baada ya Kabul kuingia mikononi mwa Taliban, ni kuwa aligundua kuwa 'hakuna muda unaofaa' kwa Marekani kuondoa majeshi yake.

> Marekani kwa miaka 10 ilipigana na majeshi ya ukombozi wa chi hiyo, kuzuia utawala wa Kikomunisti wa Vietnam ya Kaskini, usiiteke nchi yote.



Rais wa Afghanistan, Ashraf-Ghani, aliyekimbia nchi.



Kiongozi wa Taliban, Mullah Abdul Ghani Baradar

Sababu ni kuwa askari wa Afghanistan, licha ya mafunzo ya kina na kwa idadi kubwa ya askari, na silaha tele walizokuwa nazo, walikuwa hawana moyo, dhamira au nia ya kupigania nchi yao, hivyo ikawa ni vita isiyoweza kumalizika.

Wakosoaji wa kiongozi huyo wa Marekani, kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake Donald Trump alipoamua kuondoa kikosi cha Marekani mpakani mwa Syria na Uturuki kilichokuwa kinadhibiti mapigano eneo hilo kwa miaka kadhaa. Alichokosolewa Trump ni kuwa aliwasaliti watu wa Kurdi (kaskazini ya Syria) kwa wabaya wao, yaani majeshi ya Uturuki kwa upande mmoja na Syria kwa upande mwingine.

Trump alijibu kuwa walifikia makubaliano ya kusaidiana nao dhidi ya kundi la kiharamia la ISIS (Islamic State of Iraq and Syria).

Liliacha milima ya wafu, wengi wakichinjwa kwa visu, katika wimbi la uasi la mwaka 2014.

Trump alisititiza kuwa hapakuwa na makubaliano kati ya Serikali ya Marekani (wakati huo rais akiwa ni Barack Obama) na Wakurdi kuwa Marekani itawalinda milele, na ndicho kinachojirudia Afghanistan.

Ni wazi kuwa Marekani iliienda huko kuondoa utawala wa Taliban, pale iliposhambuliwa na marafiki zao wa Al Qaeda, Septemba 11, 2001. Endapo baada ya miaka 20 raia wa Afghanistan na wale wanaojiunga na jeshi ni wazi kuwa hawana morali wowote wa kulinda utawala wa kidemokrasia.

Askari na wananchi wanaona utaifa wao na mwelekeo wa kidini ni muhimu, wakibishana kutwa kucha nani bora kati ya Taliban na Marekani, hivyo umefika wakati wa kuwaachia nchi yao.

Kimsingi tishio la ugaidi dhidi ya Marekani lilishaondolewa Osama alipouawa 2011.

Kilichobaki ni kutathmini tetemeko la kisaikolojia katika nchi nyingi duniani, ambako kijeshi sasa hali ya Afghanistan siyo tena jambo la kuhangaikiwa makao makuu ya jeshi la Marekani (maarufu Pentagon).

Tatizo hilo linawaangukia wapanga sera na mikakati wa nchi jirani kama Pakistan, China, Iran, Turkmenistan na Tajikistan.

Mojawapo kati ya nchi hizo, Tajikistan, ndipo alipokimbilia Rais Ghani alipoarifiwa kuwa vikosi vya Taliban vimezingira Jiji la Kabul hali ambayo ina maana kuwa nchi hiyo na nyingine za jirani zikiona hali ni mbaya (kwa mfano kuanza kwa sheria kali, kuuawa wafuasi wa utawala uliopita, ukandamizaji kupita kiasi wa haki za binadamu na hasa wanawake) mapambano yanaweza kuanzishwa tena.

Viongozi wa Taliban wanakiri kuwa hatari hiyo ipo, hivyo wamekuwa wakieleza kuwa watataunda serikali inayoshirikisha makundi mengi, ingawa si rahisi kujua nani kati makundi ya nchi hiyo anaweza kuwa mdau anayetambuliwa na viongozi wa Taliban. Kundi ambao labda halina mjadala ni lile la wapiganaji wa Kiislamu wasio wa sharia halisi waliokuwa wanaitwa Mujahideen, wakaiondoa serikali ya Kikomunisti ya awali, lakini nao wakaondolewa na Taliban katika vita vilizopiganwa nchini humo.

Haya makundi yasiyofungamana na imani yenye uhusiano wa karibu na nchi za Magharibi hayaelekei kuwa yatapata nafasi katika meza ya mazungumzo nani aunde serikali inayofuata na malengo yake yawe nini.

Ila kwa vile hapakuwa na mbadala wa Marekani kudhibiti hali hiyo, sera ya sasa ni 'live and let live,' kushirikiana na Taliban kwa kiasi kinachowezekana, hata kama hatua zao za utawala zitakuwa shubiri kwa mataifa jirani au nyingine.

# Ruto anavyojipanga 'kutoboa' urais bila muungano kisiasa

Na Mwandishi Wetu

KENYA mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inatarajia kufanya uchaguzi mkuu mwakani, ikiwa ni hitimisho la miaka 10 ya utawala wa Rais Uhuru Kenyatta.

Uchaguzi huo utafanyika ukiwa na kumbukumbu kadhaa zilizowatenganisha na kuwafitinisha Wakenya, na nyingine zikiegemea katika kuwaimarisha na kuwaleta pamoja raia wa taifa hilo lenye uchumi mkubwa ndani ya EAC.

Yapo matukio kadhaa yanayodhihirisha nadharia mbili nilizozitaja utengamano uliowaleta Wakenya pamoja na mgawanyiko uliochochea mafarakano hasa ya kisiasa.

Itakumbukwa kwamba katika uchaguzi mkuu wa 2007 uliozua machafuko na mauaji nchini humo, wanasiasa wawili waliodaiwa kuwa na ushawishi mkubwa, Ruto na Kenyatta, walishukiwa kuwa wafadhili wa operesheni, machafuko yaliyosababisha vifo vya watu kadhaa, huku wengine maelfu wakiyahama makazi yao.

Wawili hao, Kenyatta aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu na Ruto Waziri wa Elimu wakatajwa kwenye orodha ya watuhumiwa sita walioitwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) iliyoko The Hague, Uholanzi na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Louis Moreno Ocampo, Desemba 15, 2010.

Wengine ni mwanahabari Josua arap Sang, Mkuu wa Utumishi wa Umma, Francis Muthaura (sasa ni marehemu), aliyekuwa Waziri wa Viwanda Henry Kosgey na aliyewahi kuwa Mkuu wa Polisi nchini humo, Mohammed Hussein Ali.

Kwa hali hiyo, taswira ya uchaguzi mkuu huo ukajenga misingi ya ubaguzi, chuki, uhasama na vurugu kwa Wakenya, huku Ruto anayetoka kwenye jamii ya Wakelenjing na Uhuru wa Wakikuyu, wakiwa miongoni mwa washukiwa wa udhalimu huo.

Wakati huo Ruto akiwa mbunge wa Eldoret Kaskazini alikuwa akimuunga mkono mgombea urais wa muungano wa Orange for Democratic Change (ODM), Raila Odinga wakati Kenyatta akiwa mshirika wa karibu wa Rais wa wakati huo, Mwai Kibaki wa Party of National Unit (PNU).

Hata hivyo, uhasama kati ya wawili hao ulianza kutoweka kufutia kukorofishana kati ya Ruto na Odinga, hali iliyomfanya mwanasiasa huyo mwenye uzoefu wa 'kete' za siasa na uchaguzi nchini humo na kundi kubwa la wabunge waliokuwa wanamuunga mkono, kuegemea upande wa Rais Kibaki (kwa wakati huo) alipokuwapo Kenyatta.

### TAFSIRI ZA USHIRIKA

Zipo tafsiri mbalimbali zilizotolewa na wachambuzi wa siasa za Kenya na kwingineko barani Afrika, zikielezea kwamba licha ya uhasama uliojitokeza kati ya Ruto na Kenyatta, kurejea kwao pamoja kulijijenga katika msingi wa kuepuka mashtaka yaliyokuwa yanawakabili ICC.

Kwa maana kwamba, ili Ruto aweze kutiani ipasavyo, ulihitajika ushahidi usiotiliwa shaka hasa kutoka kwa jamii ya Wakikuyu waliodaiwa 'kuumizwa' na lililokuwa 'genge' la mwanasiasa huyo.

Na hali kama hiyo ilidaiwa pia kutokea kwa Kenyatta aliyetajwa katika kashfa ya kufadhili 'magenge' kama yaliyodaiwa kuwepo kwa Ruto, likiwemo lile maarufu la Mungiki lililowaumiza zaidi watu wa jamii ya Wakalenjin.

Hivyo, kitendo cha Ruto kujitenga katika muungano wa vyama vilivyounda ODM chini ya kinara wao Odinga, kisha kujiunga na PNU ya Kibaki alipokutana na Kenyatta, kulififisha uwezekano wa kutiwa hatiani.

Hali hiyo ilitokana na hisia kwamba kama mashahidi wa jamii ya Wakalenjin anapotoka Ruto 'wangemuangamiza' Kenyatta, ni dhahiri kwamba hata wale wa kutoka jamii ya Wakikuyu 'wangemwaga mboga' dhidi ya Ruto.

### USHINDI WA JUBILEE

Wakati uchaguzi mkuu wa 2007 ukiacha makovu kwa Wakenya, uchaguzi wa 2013 ukawa wenye nafuu kwa wanasiasa hao, kutokana na kuungana pamoja kupitia muungano wa vyama vya The National Allience (TNA) cha Kenyatta na United Republican Party (URP) cha Ruto waliounda muungano wa Jubilee na kumsimamisha Kenyatta kuwania urais wakati Ruto akiwa mgombea mwenza.

Jubilee ilishinda katika uchaguzi mkuu huo na Kenyatta kuwa Rais huku Ruto akiwa Makamu wa Rais. Ndivyo ilivyo hadi sasa.

Zipo tetesi kwamba kitendo cha Kenyatta kuwania urais kilifanyika kwa makubaliano kwamba atakapotoka madarakani, amuunge mkono Ruto kupitia muungano huo, ili agombee na akishinda awe Rais wa awamu wa tano wa Kenya.

Kenyatta alishinda katika uchaguzi huo dhidi ya mgombea 'urais mzoefu' Odinga. Na hali kama hiyo ikatokea tena katika uchaguzi mkuu wa 2017 ambao hata hivyo, matokeo yake yalitenguliwa na mahakama kuu nchini humo.

Kutenguliwa kwa matokeo hayo kulikosomwa na aliyekuwa Jaji Mkuu wa Kenya, David Maraga, Septemba Mosi, 2017, kuliwezesha kufanyika kwa uchaguzi wa marudio ambao Odinga na muungano wa National Super Alliance (NASA) waliususia na hatimaye Kenyatta na Ruto wakarejea tena madarakani kwa awamu ya pili.

### MAFARAKANO YAMEIBUKA

Kama ilivyotokea kwa Odinga, Ruto akajikuta kwenye mfarakano wa kisiasa na Rais Kenyatta, huku mshindani wao, Odinga akisogea na kuwa mshirika wa karibu wa Rais Kenyatta.

Machi 9, 2018, Rais Kenyatta na Odinga walikutana ghafla na kupeana 'salaam ya mikono' maarufu kama hand shake, ikiashiria kuondoa tofauti zilizokuwapo kati yao.

Kidogo-kidogo, Rais Kenyatta akanza kukaa kando dhidi ya mshirika wake Ruto, lugha za mafumbo ya kisiasa zikatamalaki kati yao na washirika wao wa kisiasa. Wawili hao ni kama 'hawapiki chungu kimoja' leo zikiwa zimesahalia siku chache kufikia tarehe ya uchaguzi mkuu mwakani

> Machi 9, 2018, Rais Kenyatta na Odinga walikutana ghafla na kupeana 'salaam ya mikono' maarufu kama hand shake, ikiashiria kuondoa tofauti zilizokuwapo kati yao.



Naibu Rais wa Kenya, William Ruto. **PICHA: MTANDAO**

Sasa Kenya inaelekea katika uchaguzi mkuu wa mwakani, wakati ambapo mafungamano kati ya Rais Kenyatta na Ruto yanatajwa kumeguka, huku kiongozi huyo wa taifa la Kenya akizidi kuwa karibu na Odinga.

Inaweza kuchukuliwa kama jambo lisilo jema kisiasa, lakini kwa Kenya, hali kama hiyo imeshuhudiwa mara kadhaa kwa wanasiasa wakati ambapo nchi hiyo inaelekea kwenye uchaguzi mkuu.

### RUTO KUSIMAMA PEKEE

Suala la msingi linalosubiriwa kwa hamu katika uchaguzi mkuu wa Kenya mwakani, ni namna ambavyo Kenya inaweza kuingia kwenye mfumo mpya wa kisiasa na utawala, ikiwa hatua ya Ruto kukataa kata-kata kuwa na muungano wa vyama vya siasa, ili ashinde katika uchaguzi huo itafanikiwa.

Ruto ameshaweka wazi kwamba katika uchaguzi huo , hawezi kuingia kwa kuhusisha muungano wa vyama, bali anayetaka kumuunga mkono anapaswa kujiunga katika chama chake kipya cha United Democratic Alliance (UDA).

Hivyo, kama azma hiyo itafanikiwa ni wazi kwamba Ruto atairejesha Kenya kwenye mfumo wa chama kimoja kinachotawala. Lakini kama hilo litakuwa gumu kufikia azma yake ya kuingia ikulu, ni wazi kwamba itafunga milango kwa wanasiasa wengine kutumia mfumo huo.

Lakini Ruto kutoshirikisha vyama vingi kwenye muungano wa kumuunga mkono, ili ashinde uchaguzi mkuu wa mwakani, haupaswi kubezwa ama kupuuzwa.

Ruto anatambua historia ya wanasiasa wa nchini humo 'kugeukana' kila unapokaribia uchaguzi mkuu. Kwa maana matukio ya aina hiyo yametokea kwa miaka mingi ambayo mwanasiasa huyo Ruto ameshiriki.

Ndiyo maana, inawezekana kwamba Ruto anahitaji 'kugeukwa' katika uchaguzi huo na njia anayoiona inafaa kumfikisha kwenye kilele cha ushindi ni kuwa na timu moja ya chama kimoja, inayonuwia mamoja katika kukabiliana na ushindani wa kisiasa kuekelea uchaguzi mkuu wa mwakani.

Kama Ruto atafanikiwa kufikia azma hiyo, ni wazi kwamba anaweza kujenga chama imara chenye utii kwa kiongozi mkuu wa nchi, na hivyo kurahisisha hatua za udhibiti wa kila msaidizi wa Rais atakayejaribu kwenda kinyume na matarajio ya walio madarakani.

Lakini kwa ujumla wake, uchaguzi mkuu huo wa Kenya unangojewa kwa hamu na mataifa kadhaa duniani, huku ukichochewa na hatua ya Ruto aliye Makamu wa Rais kushikilia msimamo wa kuwania kiti cha urais ambacho hivi sasa kinashikiliwa na Rais Kenyatta.

HAKAINDE HICHILEMA

# Mhanga wa uhaini ‘aliyempiga’ rungu kwa kishindo Rais Lungu

**Na Christina Mwakangale**

## • Bin Gadaffi anaendeleza historia upinzani kuwachomoa watawala Ikulu

HAKAINDE Hichilema almaarufu HH, ndiye Rais mteuliwa wa Zambia. Ni kiongozi wa chama cha upinzani cha National Development (UPND), Jumatatu wiki hii ametangazwa na Tume ya Uchaguzi wa Zambia (ECZ), kuwa mshindi wa urais baada ya kushinda kwa kishindo kwenye uchaguzi uliofanyika wiki iliyopita. Na Rais aliye madarakani Edgar Lungu, amekubali kushindwa.

Hichilema ambaye aligombea kiti hicho kwa awamu tano na kuangushwa, alikuwa kati ya wagombea 16, ambao walikuwa wanawania urais kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu na anaibuka kidedea baada ya kuzoa kura 2,810,777 huku Lungu akijipatia 1, 814, 201 ikiwa ni tofauti ya kura 996, 576, zilizopigwa kwenye uchaguzi mkuu, Alhamisi iliyopita.

Rais mpya ni mhanga wa kesi ya uhaini iliyofunguliwa Aprili 2017. Wakati huo aliwekwa rumande akikabiliwa na kesi ya uhaini ya kudaiwa kutaka kuiondoa serikali iliyokuwa madarakani na alihukumiwa kifungo cha miezi minne jela, kabla ya kufutiwa mashitaka kupitia kipengele cha ‘Nolle prosequi’ na Mwanasheria Mkuu wa Zambia.

Historia ya Zambia ya marais walioongoza muhula mmoja na kuondoshwa na upinzani muhula wa pili si ngeni, isipokuwa Muasisi Hayati Kenneth Kaunda aliyedumu madarakani kwa miongo takribani mitatu akiondolewa kwenye sanduku la kura na Fredrick Chiluba.

Chiluba naye aliangushwa na Levy Mwanawasa, kisha Rupiah Banda akaondoshwa kwa kura na Michael Sata almaarufu King Cobra, na sasa Lungu ameondolewa kwa kura nyingi baada ya Hakainde Hichilema kumtoa kwa kishindo. Kadhalika, Zambia ndiyo nchi pekee ambayo marais wawili walifia madarakani, ambao ni Levy Mwanawassa na Michael Satta na warithi wao walikuja kuondolewa madarakani kupitia uchaguzi mkuu



Hakainde Hichilema almaarufu HH.



Edgar Lungu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> “Zambia ndiyo nchi pekee ambayo marais wawili walifia madarakani, ambao ni Levy Mwanawassa na Michael Satta na warithi wao walikuja kuondolewa madarakani.

### KILICHOJIRI UCHAGUZI MKUU

Uchaguzi mkuu uliofanyika Alhamisi iliyopita, ulishuhudia wagombea 16 waliowania kiti cha urais, wakati zaidi ya watu 7,000,000 sawa na asilimia 83 ya wenye umri wa kupiga kura Zambia, wakijiandikisha kwenye orodha ya wapigakura.

Upinzani mkali ulikuwapo kati ya wagombea wakuu wawili, ambao ni Lungu wa chama cha Patriotic Front -PF na mgombea mkuu wa upinzani Hichilema wa UPND.

Lungu, ambaye aliingia madarakani mwaka 2015, baada ya kupiga kura jijini Lusaka, alikielezea chama chake cha Patriotic Front akisema: Sisi ni timu iliyoshinda’.” Akiwahimiza watu kujitokeza kupiga kura.

“Maoni yangu ni kwamba Wazambia wako tayari kupiga kura na wamejitokeza kwa wingi, niliona foleni kadhaa nilipokuwa nikija hapa, hii inakumbusha kile kilichotokea mwaka 2011, wakati watu walipojitokeza kwa wingi na ninatumai kuwa wengi zaidi watakuja kupiga kura. Mgombea bora ashinde.”

Hichilema (59), hii ni mara ya sita kuwania kiti cha urais katika nchi hiyo iliyo na wakazi milioni 18 na baada ya ushindi anaahidi, akichaguliwa ataweka misingi ya kuwavutia wawekezaji na kusimamia kikamilifu uchumi wa Zambia kutokana kuwapo madai ya ufisadi.

Hichilema ni mfanyabiashara anayewaambia waandishi wa habari kabla ya kutangazwa mshindi kwamba, uchaguzi huo unapaswa kusababisha mabadiliko ya serikali, akiongeza kuwa Zambia ilishuhudia ukuaji mkubwa wa uchumi muongo mmoja uliopita, hivi sasa inakabiliwa na mfumuko mkubwa wa bei, deni la taifa linaongezeka na madai ya rushwa iliyokithiri.

“Natangaza kwamba Hichilema ndiye Rais wa Zambia, anasema Mwenyekiti wa tume hiyo, Esau Chulu katika kituo cha kutoa matokeo kilichopo mjini Lusaka.

### LUNGU AKOSOA

Rais Lungu kabla ya kutangazwa matokeo rasmi ya uchaguzi huo mkuu, alitoa taarifa kwamba, uchaguzi haukuwa huru na wa haki na kudai kuwa mawakala wa chama tawala cha ‘Patriotic Front‘ walifukuzwa katika vituo vya kupiga kura, hali iliyowafanya kushindwa kulinda kura zao.

Lungu pia alidai mikoa mitatu ambako chama chake kimeshindwa, upigaji kura ulikumbwa na vurugu na ndiko matumaini makubwa yalikoegemea, kwamba angepata kura za kutosha. Hata hivyo awali matokeo katika maeneo hayo, ambayo yanatajwa kuwa ni ngome za Lungu, yaliashiria kuwa Hichilema amepata uungwaji mkono mkubwa katika ngome za mpinzani wake, tofauti na uchaguzi wa mwaka 2016, uliogubikwa na madai ya wizi wa kura.

Wanajeshi waliotanda katika barabara na ulinzi mkali ukiwekwa katika kituo cha kutangazia matokeo mapema Jumapili. Aidha, baadhi ya wagombea urais wamekubali kushindwa na kumpongeza Hakainde Hichilema, kiongozi wa chama cha ‘United Party for National Development‘ kwa kuchukua ushindi mapema katika uchaguzi huo.

Huku matokeo ya Tume ya Uchaguzi Zambia, yakimtangaza Hichilema kuwa mshindi, Mamlaka ya Mawasiliano na Teknolojia Zambia, imepelekwa mahakamani kwa kudhibiti huduma za intaneti na mitandao ya kijamii. Mahakama Kuu ya Zambia iliamuru marufuku hiyo kuondolewa mara moja.

### HICHILEMA NI NANI?

Hakainde Hichilema alizaliwa Juni 4, 1962, Wilaya ya Monze, Zambia na ni mfanyabiashara na kiongozi wa UPND tangu 2006 na ushindi wa sasa unakuja baada ya kuwania urais mara tano mwaka 2006, 2008, 2011, 2015 na 2016 bila mafaniko.

Ni mchumi mwenye shahada ya uchumi, biashara na utawala aliyehitimu Chuo Kikuu cha Zambia mwaka 1986 na kisha kupata shahada ya uzamili katika masomo hayo Chuo Kikuu Birmingham nchini Uingereza.

Amewahi kuwa Ofisa Mkuu wa Coopers and Lybrand Zambia mwaka 1994 hadi 1998 kisha Grant Thornton Zambia mwaka 1998 hadi 2006. Baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa UPND Anderson Mazoka mwaka 2006, alichaguliwa kushika wadhifa huo, pia aliwahi kukiongoza Chama cha United Democratic Alliance (UDA) ambacho ni muungano wa vyama vitatu.

Mwaka 2006 kwenye uchaguzi mkuu, Hichilema uliwania urais kupitia UDA dhidi ya Rais Levy Mwanawasa wa Chama cha Movement for Multiparty Democracy kadhalika mgombea mwingine wa kiti hicho alitoka chama cha Patriotic Front, Michael Sata.

Kwenye uchaguzi huo uliofanywa Septemba 28, 2006, Hichilema alishika nafasi ya tatu akipata kura kwa asilimia 25 ya kura zote zilizopigwa. Kupitia chama cha UPND mwaka 2008 baada ya kifo cha Levy Mwanawasa, aligombea na kushika nafasi ya tatu akipata asilimia 19.7.

Juni mwaka 2009, Hichilema’ na Michael Sata waliungana na kushiriki pamoja urais katika uchaguzi wa mwaka 2011 ingawa hawakufanikiwa. Ilipofika 2015 alikuwa kati ya wagombea urais wakuu, na uchaguzi uliofanyika Januari mwaka huo alipata kura 27,757 sawa na asilimia 1.66 dhidi ya chama tawala pia 2016 aliangushwa katika uchaguzi mkuu.

**MTANDAO**

## Viongozi wa vyama vya siasa wanapotajiwa mbinu kufanikiwa

**INATOKA UK.11**

wa migogoro zipo njia mbili ikiwamo kukutana na upande mmoja kwa siri, kisha upande wa pili, ili kupata picha halisi ya mgogoro na kutafuta ufumbuzi na baadaye pande zote zinazohusika.

“Rais anaweza kufanya hilo au kukutana na vyama vyote kwa pamoja katika ahadi yake ya kutaka kukutana navyo, lakini jambo la msingi ni wahusika kutanguliza maslahi ya taifa si ya vyama vyao,” anasema.

WASIKILIZWE

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk.Hellen Kijo-Bisimba, anasema kwa vyovyote vile, viongozi wa chama hicho wana sababu zao za msingi zinazopaswa kusikilizwa kwanza.

“Nakumbuka, wao ndiyo walikuwa wa mwanzo kuomba kukutana Rais kwa vile walikuwa na ajenda yao na tunasikia walipewa jibu kuwa wasubiri tarehe ya kukutana na kiongozi wa nchi,” anasema Dk. Kijo-Bisimba.

Anasema, huenda ni kutaka wamalize madai yao au ajenda ambayo inaweza isifanane na ya viongozi wa vyama vingine, na kwamba haoni kama uamuzi huo ni tatizo.





# Leseni kutolewa kupitia mtandao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imejipanga kuanza kutoa vitabu na leseni za biashara kwa njia ya mtandao ili kukomesha tabia ya maofisa biashara kughushi leseni.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, alisema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tano ya maofisa hao kutoka mikoa ya Morogoro, Singida na Dodoma kuhusu sheria ya leseni za biashara.

Alisema kuna baadhi ya maofisa wamekuwa wakighushi vitabu na leseni jambo ambalo ni kosa kisheria na vinahujumu uchumi.

"Kuna halmashauri ofisa biashara wake alifoji vitabu vya risiti na mwisho wa siku alikamatwa. Maendeleo hayataki uongo uongo, ili kuepukana na haya sasa tunataka kuweka mfumo mzuri wa kuchukua vitabu na leseni kwa njia ya mtandao," alisema.

Pia alisema maofisa hao wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwatembelea wafanyabiashara katika maeneo yao na kuwapa elimu ikiwamo

ya ulipaji wa kodi na si kuwabugudhi ili wasijenge uadui.

"Najua kuna sheria za biashara lakini wakati mwingine lazima mwongozwe na busara ili kupata matokeo yaliyo chanya kwani kufunga

biashara si suluhisho na pia ilishapitwa na wakati," alisema Nyaisa.

Alisema ni vyema kutanguliza busara ili kuwa na matokeo chanya ya kile ambacho wamekusudia kukifanya.

Aidha, alisema serikali haifanyi biashara bali inatoa huduma, hivyo kupitia mafunzo hayo anaamini maofisa biashara watabadilika na

watapata fikra mpya ambapo wataenda kutumika katika kuongoza biashara.

"Kuna maofisa biashara wanapiga sana hela. Wawekezaji wanakuja lakini

mnawapiga ikiwamo kuwafanyia urasimu wakati nyie ndio mlitakiwa kuwapa ushirikiano mkubwa, "alisema Nyaisa.

Mtendaji Mkuu huyo aliwataka kuwatembelea wafanyabiashara na kutoa elimu kwao kuhusu madhara ya kufanya biashara bila leseni.

"Mfanyabiashara asipokuwa na leseni hawezi kuendelea kwa kuwa hatoweza kupata mkopo kutoka benki lakini pia hakuna biashara inayokuwa yenyewe bila mkopo. Hata kama una mshahara bado haitoshi kuikuza biashara yako bila mkopo," alisema Nyaisa.

Alisema hakuna aliyetajirika kwa fedha ya mshahara, wala binafsi hivyo wanahitaji wafanyabiashara wanaokua.

# Serikali kusomesha wahadhiri 623

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kusomesha wahadhiri 623 na kuanzisha programu mpya 290 ili kuboresha ubora wa elimu ya juu nchini.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdee, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya serikali kwenye elimu ya juu katika Chuo Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa (MUCE) ambacho ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alisema wahadhiri hao watasomeshwa kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi ambao unaanza mwaka huu wa fedha 2021/22 na utagharimu Sh. bilioni 985.

"Agosti 19, mwaka huu, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, atatia saini makubaliano na Benki ya Dunia kwa ajili ya mradi huu na utatekelezwa katika vyuo vyote vya umma pamoja na vyuo vishiriki, Tume ya Vyuo Vikuu, mafunzo kwa wafanyakazi walio kazini," alisema.

Alibainisha kuwa fedha hizo pamoja na kusaidia ujenzi wa miundombinu pia zitapelekwa kwenye mafunzo kwa watumishi ili kuendana na wakati.

"Tutasomesha wahadhiri 623 kwa shahada ya uzamivu na 477 wa shahada ya umahiri. Tutaanzisha programu mpya 290 na tutaongeza udahili wa wanafunzi lengo likiwa kuwabeba hawa wanafunzi ambao wanaongezeka," alisema.

Akizungumzia mafanikio mbalimbali ya elimu ya juu, Prof. Mdee alisema kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita imesomesha wahadhiri 746 nje ya nchi kwa ngazi mbalimbali ikiwamo shahada ya pili na ya tatu.

"Katika miaka mitano 2015-2020, wizara imesomesha wahadhiri 746 nje ya nchi. Kati ya hao, waliosoma shahada ya uzamivu ni 552 na shahada ya umahiri ni 194," alisema.

Kuhusu mikopo, alisema kwa mwaka wa masomo unaotarajiwa kuanza Oktoba, mwaka huu, serikali imeongeza bajeti hadi Sh. bilioni 570 ikidhamiria kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi walioomba wenye sifa.



Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Elibariki Masuke (wanne kulia), akikabidhi msaada wa vifaa vya ujenzi vikiwamo mabati 240, mifuko 120 ya saruji na kilo 30 za misumari ya bati kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga, Grace Quintine, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa madarasa 20 katika Shule ya Msingi Nazareth, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma. Wengine ni maofisa wa benki hiyo na viongozi kutoka serikalini na kamati ya shule hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wabunge wachangamkia chanjo corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameanza kupata chanjo ya corona huku mwamko ukiwa mkubwa kutokana na kuhamasishana umuhimu wa chanjo hiyo.

Nipashe jana ilitinga katika viwanja vya bunge na kushuhudia wabunge wakipata chanjo hiyo kwenye eneo maalum lililoandaliwa.

Akizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kupata chanjo, Mbunge wa Singida Mjini, Mussa Sima, alisema wabunge sasa wameanza vikao vya kamati za bunge, huduma hiyo imesogezwa karibu nao na wanaendelea kuhamasishana ili kupata chanjo hiyo.

Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira, alisema kwenye kamati yao, wanahamasishana kwenda kupata chanjo na wamekuwa wakisindikizana kuchanjwa.

"Mbunge akiingia tunamuuliza kama amechanja na kama bado tunamsindikiza anaenda kupata chanjo, tunarudi kuendelea na kikao," alisema.

Mbunge wa Mwanga, Joseph Tadayo, alisema corona ni ugonjwa kama magonjwa mengine na sababu zake wataalamu wameeleza na utafiti umefanywa na chanjo imepatikana.

"Ubora wa chanjo umeelezwa, mimi nachukulia jambo hili ni zuri na wataalamu ambao wamefikia hatua hiyo tuwapongeze. Watu wengi wamechanjwa na Prof. (Mohamed) Janabi (Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete- JKCI) alishasema madhara ya chanjo ni kitu ambacho hakipo," alisema.

Tadayo alitoa wito kwa wananchi wenye nafasi ya kuchanjwa waende kuchanjwa.

"Mtu ana uhuru wa kuchanja au kutochanja lakini kusimama kuanza kupiga kelele kuwashawishi wengine wasichanje nadhani hii si sawa. Watanzania wana utashi wao wakiambiwa ni hiari wanapima kwa mujibu wa matokeo kwa waliochanjwa," alisema. Alibainisha kuwa matokeo aliyoyaona kwa waliochanjwa ni mazuri na hajapata maudhi yoyote tangu amechanja.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, alishauri wananchi wafuate maelekezo ya wataalamu wa afya ili kujikinga na ugonjwa huo.

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi, ambaye ni Katibu wa Wabunge wa CCM, alisema katika mkusanyiko wa bunge wanakutana na watu mbalimbali ni vyema kujikinga.

"Nimechanja kwa hiari bila kushurutishwa na hata wangekuwa na aina zote za chanjo mimi ningechanja," alisema.



# Wawekezaji walalamikia gharama za umeme

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

WAWEKEZAJI wa viwanda vya kuchenjua dhahabu katika Mji Mdogo wa Makongolosi, wamelalamikia gharama kubwa ya umeme kwenye uendeshaji wa viwanda hivyo wakidai kuwa ni kubwa na sio rafiki kwenye uwekezaji.

Aidha, wawekezaji hao wamedai kuwa wanalazimika kuvuta umeme kwa gharama zao ikiwamo kununua transfoma, nyaya na nguzo kutokana na Shirika la Umeme (TANESCO) kutowapelekea huduma hiyo kwa wakati. Walitoa malalamiko hayo juzi wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya pamoja na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), zilipofanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani Chunya.

Mmoja wa wawekezaji hao, Fidel Ntanyinya ambaye ni mmiliki wa Kampuni ya FINTA INU .CO, alisema pamoja na gharama kubwa ya ankara za umeme wanazolipa, lakini huduma hiyo siyo ya uhakika kutokana na kukatika mara kwa mara.

"Umeme ukikatika tunalazimika kutumia jenereta ambazo huongeza gharama za uendeshaji, kuna kipindi wakati wa ujenzi wa barabara ya Chunya-Makongolosi tulipata shida sana maana walikuwa wanahamisha nguzo na hivyo kusababisha tutumie gharama kubwa kwenye uendeshaji," alisema Ntanyinya.

Alisema kwenye uwekezaji huo wanategemea zaidi mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya NMB ambayo alisema imekuwa ikiwakopesha, lakini tatizo lililopo maeneo yao mengi hayajarasimishwa na hayana hatimiliki na hivyo baadhi ya benki huwa hazikubali kuwakopesha.

Mwakilishi wa Kiwanda cha Kindai Elution, Nazar Haydar, alisema wanalipa zaidi ya Sh. milioni 8.5 kila mwezi kwa ajili ya umeme wa kuendeshea kiwanda hicho jambo ambalo alidai ni hasara kwao.

Alisema pamoja na gharama hizo, lakini umeme huo waliuvuta wenyewe kwa gharama ya Sh. milioni 40 ikiwa ni pamoja na kununua Transfoma na vifaa vingine.

"TANESCO walisema wao kama watatuletea transfoma itakuwa kwa kuchelewa sana na ndio maana sisi tukaamua kutumia gharama zetu wenyewe, lakini viwanda hivi ni kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo," alisema Haydar.

Alisema kwenye viwanda hivyo wameajiri idadi kubwa ya vijana ambao awali walikuwa hawana ajira, lakini kutokana na gharama za umeme wakati mwingine huwa wanatamani kupunguza.

Kutokana na malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alimtaka Meneja wa TANESCO Wilaya ya Chunya ama mwakilishi wake atolee majibu lakini hakukuwa na mtu yeyote wa shirika hilo kwenye ziara hiyo.

Homera aliagiza Meneja wa Shirika hilo wa Wilaya kujieleza ndani ya siku saba kwanini hakuhudhuria ziara hiyo wakati alikuwa na taarifa pamoja na kutoa majibu ya malalamiko ya wawekezaji.

"Hizi zitakuwa ni dharau kubwa na sasa lazima tuanze kuadabishana, sasa haya malalamiko ya wawekezaji wetu anajibu nani, naomba haya malalamiko tuyachukuwe lakini huyu meneja lazima ajieleze," alisema Homera.

Alisema kitendo cha kero za wawekezaji kutotatuliwa kwa wakati kitasababisha baadhi yao kukimbia na kwenda kuwekeza maeneo mengine na hivyo kuikosesha serikali mapato.

Hata hivyo, aliwataka wawekezaji hao kushirikiana na serikali kudhibiti utoroshaji wa madini kwa wao wenyewe kutoshiriki vitendo hivyo haramu.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alisema wilaya hiyo kwa mwezi inakusanya zaidi ya kilo 300 za dhahabu inayozalishwa kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema viwanda vya kuchenjua dhahabu wilayani humo vipo zaidi ya 30 na kwamba idara zote za serikali huwa zinashiriki kwenye usimamizi wakati wa uchenjuaji ili kuepusha udanganyifu.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wapili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya kichenjua dhahabu ya Finta INU.Co, Fidel Ntanyinya (kulia), kuhusu dhahabu inavyochenjuliwa wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) zilipotembelea kiwanda cha mwekezaji huyo, wilayani Chunya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wajitokeza kupata chanjo ya corona

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameendelea kujitokeza kwenye vituo vya kutolea chanjo ya kujikinga dhidi ya corona ili kupata huduma hiyo.

Nipashe ilitembelea vituo vya kutolea huduma hiyo katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya Kitengo cha Wazazi na katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya na kushuhudia makundi mbalimbali ya watu yakipata chanjo hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, John Mwankota, alisema awali alikuwa haamini chanjo hiyo, kutokana na uvumi uliokuwa unasambaa mitaani kwamba zina madhara kwa binadamu ikiwamo kuganda kwa damu na kifo.

Alisema aliamini kwamba chanjo hiyo ni salama baada ya kushuhudia Rais, Samia Suluhu Hassan akichomwa pamoja na baadhi ya viongozi wa serikali na wa dini.

"Ukikaa mitaani unasikia mengi sana, lakini mimi naamini rais hawezi kutuletea kitu cha kutuua, siamini kwamba yeye alichoma chanjo ambayo ina madhara, kwa hiyo mimi nimeamua nichanje ili kujiweka salama," alisema Mwankota.

Naye Mariam Mwantobe alisema alihamasishwa na rafiki yake ambaye ni mtumishi wa afya katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali, ambaye alimwaminisha kuwa chanjo hiyo ni nzuri na haina shida yoyote.

Alisema baada ya uchomwa alikuwa hana tatizo lolote na kwamba hata maumivu aliyopata wakati anachomwa yalikuwa ya kawaida na hivyo akawataka wananchi wengine kwenda kuchanjwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, alisema mkoa huo ulipokea dozi za awali 50,000 ambazo zimegawanywa katika wilaya zote za Mkoa huo, na kwamba i idadi kubwa ya wananchi wamejitokeza kuchanjwa.

Alisema kwa sasa mwamko umekuwa mkubwa kuliko ilivyokuwa awali, ambapo wananchi wengi walikuwa hawaamini kuwa chanjo hiyo ni salama.

Hata hivyo, aliwataka wananchi waendelee kuchukua tahadhari za kujikinga na virusi hivyo kwa kuepuka mikusanyiko, kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono na kuvaa barakoa.

# Ujenzi wa miundombinu kwa vifaa hafifu waonywa

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

MKOA wa Mbeya umewatahadharisha watendaji wa halmashauri wanaojenga miundombinu ya umma kwa kutumia vifaa vyenye ubora hafifu kuwa itawachukulia hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa tahadhari hiyo wilayani Chunya wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi zilipofanya ziara ya kukagua miradi itakayotembelewa na Mwenge wa Uhuru.

Alitoa tahadhari hiyo baada ya kubaini uwapo wa mkanganyiko wa kiwango cha ubora wa saruji inayotumika kwenye ujenzi wa jengo la soko la madini la wachimbaji wadogo wilayani Chunya lililopo katika Kata ya Mbugani linalotarajiwa kuwa na vyumba zaidi ya 50.

Kwenye taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Mkuu wa Idara ya Manunuzi wa Halmashauri ya Chunya, Salome Lyimo, alisema wanatumia saruji yenye ubora wa 32.5 kutokana na ushauri waliopewa na Mhandisi wa Halmashauri.

Hata hivyo, yaliibuka mabishano kati ya Salome na Mhandisi wa Halmashauri hiyo, Joseph Halinga ambaye alidai inatumika saruji yenye ubora wa 42.5 kama ilivyo kwenye jengo la halmashauri ambalo pia linaendelea kujengwa.

"Kwenye hili jengo tunatumia saruji ya 32.5, wakati kwenye lile la halmashauri tunatumia ya 42.5, lakini bati zote tunazotumia kwenye majengo haya ni ya 'gage' 28," alisema Lyimo.

Baada ya maelezo hayo ya Ofisa Manunuzi na Mhandisi wa Halmashauri, Homera alionyesha kutofurahishwa, akisema kuwa kwenye miongozo majengo yote ya serikali yanatakiwa kujengwa kwa saruji yenye ubora wa 42.5.

"Jengo kubwa kama hili mnatumia saruji ya 32.5 nani aliyewaambia? Likija kuwaangukia watu mtafanyaje? Sasa nawaambieni hata mabati ole wenu mje mtuezekee ya ajabu ajabu, yatakapokuwa yanapauka nanyi mtakuwa mnapauka," alisema Homera.

Kwa upande wake Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Christopher Palanjo, alisikitishwa na idara ya manunuzi ya Wilaya ya Chunya kununua matofali ya kujengea majengo ya Serikali Mbeya Mjini wakati kuna uwezekano wa vifaa hivyo kununuliwa wilayani humo.

Palanjo alisema kitendo cha kununua matofali hayo Mbeya Mjini kinasababisha gharama za miradi hiyo kuongezeka ambapo alisema wanalazimika kununua tofali moja kwa Sh. 15,000 na hivyo akawataka kuwa wabunifu.

Alisema ili kupunguza gharama hizo, Halmashauri ya Chunya inatakiwa kutumia sehemu ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wajasiliamali vijana ili wafyatuwe matofali wilayani humo na serikali iyanunuwe kwa ajili ya miradi ya umma.



# Hemed ataka nidhamu kwa watumishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetakiwa kusimamia vyema majukumu yake katika sehemu za kazi ili kurejesha nidhamu kwa watumishi wake.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kuimarisha utendaji kazi katika taasisi za serikali.

Alisema uongozi wa wizara unatakiwa kusimamia kwa karibu na kurugenzi zake kuhakikisha ufanisi unapatikana kwa wananchi wanaofika kupata huduma katika vituo vya afya.

Hemed alisema kuna kila sababu kwa wizara hiyo kuwa makini katika utendaji wa kazi zake za kila siku na ripoti zinaonyesha imo katika orodha ya taasisi zisizozingatia nidhamu katika matumizi ya fedha za serikali.

Katika kurejesha nidhamu ya matumizi ya fedha za serikali alimwagiza Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinavyonunuliwa viendane na thamani halisi ya fedha inayotumika.

Alisema serikali inayoongozwa na Dk. Hussein Mwinyi imedhamiria kuimarisha huduma zinazotolewa na sekta ya afya sambamba na kudhibiti matumizi ya fedha za serikali na itakapobidi haitasita kubadilisha baadhi ya sheria ili kufanikisha lengo hilo la serikali.

Akikagua maabara ya vipimo vya vinasaba mbalimbali, Hemed aliuagiza uongozi wa wizara hiyo kutoa kipaumbele maalum kwa kitengo hicho kutokana na umuhimu wake kwa kutatua changamoto za vifaa pamoja na kuangalia maslahi ya wafanyakazi na watendaji kutokana na kufanya kazi katika mazingira hatarishi.

Aidha, Makamu wa Pili huyo aliwataka viongozi wanaosimamia kipimo cha vinasaba vya corona, kuacha kuwaharakisha wataalamu wanaofanya vipimo hivyo ili kutoa majibu sahihi kwa sampuli zinazowasilishwa katika maabara hiyo.

Hemed alisikitishwa kwa kusuasua kwa huduma ya upatikanaji wa mashuka kwa wakati kulikosababishwa na kuharibika kwa kifaa cha mashine ya kufulia, kifaa ambacho gharama yake Sh. 400,000.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Dk. Msafiri Marijani, alisema mbali na jitihada zinazochukuliwa na wataalamu katika hospitali hiyo, lakini wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo upungufu wa wataalamu wa kada mbalimbali, uhaba wa vyumba vya upasuaji na upungufu wa vitendanishi kwa ajili ya kufanya vipimo katika maabara.

Ofisa Muuguzi Mkuu, Hamida Hamid, alisema hospitali hiyo imekuwa ikizidiwa na watu wengi kunakosababishwa na wananchi wengi kukiuka taratibu kwa kutoanzia kupata huduma katika vituo vyao vya karibu katika sehemu wanazoishi.

## SMZ yapiga marufuku mabweni shule za msingi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis Juma, amepiga marufuku kuwapo kwa mabweni ya wanafunzi wa shule za msingi za binafsi na serikali.

Amesema amechukua uamuzi huo kutokana na kukithiri vitendo vya udhalilishaji katika mabweni hayo, hivyo kuleta athari kubwa kwa jamii.

Akizungumza wakati wa mkutano wa pamoja na walimu wakuu wa shule binafsi, alisema vitendo vya udhalilishaji vimekuwa kero kwa jamii, hivyo ni vyema kushirikiana ili kupunguza au kuondoa kabisa vitendo hivyo.

Kwa mujibu wa katibu mkuu, wizara inatarajia kuanzisha kitengo maalum cha shule binafsi kwa lengo la kusaidia kutatua matatizo mbalimbali yanayozikabili hivyo ni vyema kutoa ushirikiano ili kufanikisha suala hilo.

Alisema hatua hiyo pia itatoa fursa za kutoa ushauri kwa lengo la kuondoa matatizo na dhana mbaya kwa shule binafsi.

Shule binafsi, alisema bado zina mchango mkubwa wa kutoa elimu kwa watoto kwa kuisaidia serikali juu ya jukumu hilo, kama serikali ilivyotoa ruhusu juu na kuzisajili skuli za binafsi kuendeleza elimu.

Naye Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khalid Salum Waziri, alisema mkutano huo una lengo la kuleta mabadiliko kati ya shule binafsi na wizara katika utoaji wa huduma bora za elimu.

Alisema kuna tatizo kwa baadhi ya shule binafsi zinakataa kutoa ushirikiano katika masuala ya utoaji wa data hali ambayo inaleta tatizo wakati wanapopanga mipango yao katika kutoa huduma za kielimu katika shule.

Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari, Asya Iddi Issa, aliwataka walimu wakuu hao wa shule binafsi kutowafukuza wanafunzi kwa sababu za kufeli au kutokuwa na viwango vya ufaulu na badala yake wakae na wazazi kwa lengo la kutafuta njia mbadala ili kuwasaidia kufanya vizuri.

Alisema imekuwa tabia kwa baadhi ya walimu wa shule binafsi kuwafukuza watoto kwa madai ya kuweka rekodi mbaya za ufaulu katika shule zao jambo ambalo linawanyima fursa watoto katika kusoma.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kulia), akikabidhiwa boksi la dawa na Balozi Mdogo wa China aliyepo Zanzibar, Zhang Zhisheng, ikiwa ni msaada kutoka kwa serikali ya watu wa China katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri Mazrui aahidi ushirikiano na China

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, ameahidi kudumisha ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ili kuinua uchumi wa nchi.

Akizungumza na Balozi Mdogo wa China aliyeko Zanzibar na ujumbe wake, wakati akipokea msaada wa dawa kutoka Serikali ya China, Waziri Mazrui alisema serikali hizo mbili ni marafiki wa muda mrefu hivyo wataendeleza ushrikiano huo ili kuwapatia wananchi huduma bora za afya.

Pia alisema serikali ya Zanzibar inaishukuru serikali ya China kwa kushirikiana nao kwa kila hali pamoja na kuwapatia misaada mbalimbali ikiwamo dawa, madaktari na chanjo ya corona.

"Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wamekuwa wakishirikiana na sisi kwa kila hali hususani Wizara ya Afya kwa kutupatia madaktari kila mwaka na misaada mbalimbali ambayo husaidia katika kutoa huduma kwa wananchi," alisema waziri.

Mazrui alisema wizara yake imepokea dawa 165 zenye thamani ya Sh. milioni 120 kwa Unguja ambazo ni idadi sawa na dawa zilizotolewa kisiwani Pemba.

Balozi Mdogo wa China, Zhan Zhisheng, alisema serikali ya China inaahidi kuendelea kuisaidia Zanzibar na tayari imeshatia saini mkataba wa kujenga nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee, mkoani Pemba.

Zhan alieleza kufurahishwa na ushirikiano baina ya madaktari wa Zanzibar na madaktari kutoka China katika utendaji wa kazi unaosababisha kubadilishana ujuzi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Makabidhiano hayo ya dawa baina ya Wizara ya Afya Zanzibar na serikali ya China yalifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Hospitali ya Mnazi Mmoja mjini Unguja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**LEVINA R TARIMO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0238-0006** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **MRUMA GIRLS mwaka 2017**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **KIL/MOS/RB/749915/2020**

116411802

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.239/2021**

Ombi la **BONIFACE FORTUNATUS KIWALE** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **SADIKI ALFREDY MKUDE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 13/09/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 11/08/2021**

116411902

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.241/2021**

Ombi la **LUCY GEREZA KIMBWENE** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **JOSEPH GEREZA KIMBWENE**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 15/09/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 12/08/2021**

116412002

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MBUGANI CAMPS LIMITED anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina yaTOYOTA LANDCRUISER yenye namba za usajili T 239 ASH,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa ARU/ARU/RB/395636/2021**

116412502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KNONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 157 YA 2021**
**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya**
**PENDO PAULO PHILEMONI................MAREHEMU**
**DHIDI YA**
**PAULO PHILEMON MKUMBO.........MUOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 19 mwezi wa 8 mwaka 2021

**Hati hii imetolewa 10 mwezi 08 mwaka 2021**

116411702

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MARTHA BENEDICTO CHAWINGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO FIGHTER** yenye namba za usajili T 367 DFY.
Yenye Engine namba **6D16802458** na Chassis namba **FK617E510500**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi taarifa:
**TAN/RB/404234/2021**

116412702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo......MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi..........121............2021**

**Ombi la JAMALI MUSTAFA SHABANI........Ku-teuliwa**
**Msimamizi wa mirathi ya marehemu**
**.....MUSTAFA SHABANI SABUNI....**

**KwaYEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 7/9/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 17/8/2021

216412802

---

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA BUKOBA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 45.............2021**

**Msimamizi wa mirathi EDINA ATUGONZA KABYEMELA**

**Msimamizi wa mirathi ya marehemu KABYEMELA JAPHET ISHENGOMA**

Kwa kuwa Edina Atugonza Kabyemela ameleta maombi ya kusimamia mirathi ya marehemu Kabyemela Japhet Ishengoma katika mahakama hii.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 20/08/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

116412602

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EDWARD EMMANUEL MOLLEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK II** yenye namba za usajili **T 377 CRY,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**ARU/ARU/RB/395636/2021**

116412402

---

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Hichilema aahidi kufufua uchumi wa Zambia

**Lusaka,** ZAMBIA

BAADA ya ushindi mkubwa wa kiongozi wa upinzani Zambia, Hakainde Hichilema (pichani chini), dhidi ya rais aliyeko madarakani Edgar Lungu, kibarua kikubwa kilichoko sasa ni cha kufufua uchumi wa taifa hilo.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Lungu mwenye umri wa miaka 64 alimpongeza Hichilema (59), akisema kuwa ataheshimu katiba ili kuhakikisha ubadilishanaji madaraka wenye amani.

Hii ni mara ya tatu kwa chama cha upinzani kuchukua madaraka kwa njia ya amani nchini humo.

Hichilema, ambaye alikuwa mkurugenzi mkuu wa kampuni ya hesabu alisema, kipaumbele chake ni kufufua uchumi.

Zambia ni taifa la kwanza kukiri kushindwa kulipa madeni yake ya kimataifa, baada ya kutokea kwa janga la corona.

Hichilema wakati akihutubia wafuasi wake mjini Lusaka muda mfupi baada ya kupata ushindi, alisema kuwa atahakikisha kuwa anatimiza jukumu lake licha ya kuchaguliwa wakati nchi ikiwa katika hali mbaya ya kiuchumi.

Uchumi wa Zambia tayari ulikuwa ukidorora hata kabla ya janga la corona, kutokana na mfumuko wa bei za bidhaa, hali imeharibika zaidi baada ya janga hilo. **VOA**



# Uganda yapokea wakimbizi 2,000 wa Afghanistan

**Kampala,** UGANDA

UGANDA imepokea kundi la kwanza la karibu Waafghanistan 500 kati ya 2,000 waliotarajia kutua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Entebbe, jana.

Imesema kuwa itawachukua wakimbizi 2,000 wa Afghanistan, wanaokimbia mzozo nchini mwao, kufuatia ombi la Marekani.

Hii ni baada ya wanamgambo wa Taliban kuchukua uongozi wa nchi hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita na serikali iliyokuwa madarakani kuanguka.

**Uganda itakuwa nchi ya kwanza ya Afrika kuwapokea watu wanaotoroka ghasia nchini Afghanistan.**

Uganda imepongezwa kimataifa kutokana na sera yake ya kuwakaribisha wakimbizi.

Waziri wa Wakimbizi Uganda, Esther Anyakun, aliiambia BBC kwamba, Rais Museveni amekubali kuwachukua jumla ya wakimbizi 2,000 raia wa Afghanistan, baada ya kupokea ombi la Marekani.

Aliongeza kuwa watakapofika watafanyiwa vipimo vya corona na kuwekwa karantini. Vifaa na gharama zote zitashughulikiwa na serikali ya Marekani.

Uganda itakuwa nchi ya kwanza ya Afrika kuwapokea watu wanaotoroka ghasia nchini Afghanistan.

Uganda ambayo imekuwa na historia ya muda mrefu ya kuwakaribisha wakimbizi kwa sasa ni nyumbani kwa zaidi ya watu milioni moja, waliokimbia mzozo na majanga.

Wakimbizi nchini humo wanaoishi katika makazi au vijijini na wenyeji na baadhi yao wamepewa kipande cha ardhi na kuruhusiwa kufanya kazi. **BBC**




Maelfu ya watu wakivamia Uwanja wa Ndege wa Kabul nchini Afghanistan, wakitumaini kukimbia nchi baada ya Taliban kuchukua mamlaka. Watu wawili walioning'inia katika ndege ya kijeshi ya Marekani walifariki dunia, wakati ikianza kuondoka na kusababisha safari za ndege kusitishwa juzi. **PICHA: DW**

# Ndege za kijeshi zarejesha safari zake Kabul

**Kabul,** AFGHANISTAN

NDEGE za kijeshi zinazowabeba wanadiplomasia na raia kutoka Afghanistan, zimeanza tena safari zake mapema jana, siku moja baada ya maelfu ya watu kuvamia Uwanja wa Ndege wa Kabul kwa matumaini ya kukimbia nchi.

Ripoti zinasema kuwa idadi ya raia imepungua katika uwanja wa ndege wa Kabul, siku moja baada ya kutokea tafrani wakati maelfu ya watu walipouvamia uwanja huo wa ndege kwa matumaini ya kukimbia nchi.

Wanajeshi wa Marekani walijaribu kutawanya umati huo kwa kufyatua risasi, huku wengi wao wakijaribu kuning'inia katika ndege ya kijeshi ya Marekani wakati ikianza kuondoka.

Hali hiyo ilisababisha safari za ndege kusitishwa juzi, wakati watu watano walipouawa ingawa haikuwa wazi ikiwa walipigwa risasi au walikufa kwa sababu ya mkanyagano.

Ripoti nyingine za vyombo vya habari zinasema kuwa watu wawili walianguka kutoka pembeni mwa ndege hiyo baada ya kupaa na kufariki.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Ujerumani, ilisema ndege yake ya kijeshi iliyoondoka Kabul juzi jioni, ilifanikiwa kuwabeba watu saba tu.

Msemaji wa wizara hiyo aliongeza kuwa "hapakuwa na uhakika jana usiku kwamba raia zaidi wa Ujerumani na watu wengine wanaotakiwa kuhamishwa kama wangeweza kufika uwanja wa ndege bila ya ulinzi wa wanajeshi wa Ujerumani."

Mwandishi mmoja wa Afghanistan aliripoti kuwa baadhi ya shughuli zimeanza kurejea kawaida.

"Nimetembea katika maeneo ya mjini asubuhi hii na kuna ulinzi wa Taliban katika majengo ya serikali kama ikulu na wizara ya ulinzi. Kwa nyongeza ni kuwa baadhi ya maeneo ya umma yamefunguliwa.

"Shule zimeanza masomo na taasisi nyingi za umma zimefunguliwa tena. Kila mmoja anapenda amani na utulivu wa kudumu na wana matumaini kwamba kila upande utajiunga katika serikali ambayo ni jumuishi."

Wakati huo huo, kundi la Taliban limetangaza msamaha kote Afghanistan na kuwahimiza wanawake kujiunga na serikali yake na kujaribu kutuliza hali katika mji mkuu wa Kabul baada ya ghasia zilizoshuhudiwa katika uwanja wa ndege.

Kauli hiyo imetolewa na Enamullah Samangani, mwanachama katika tume ya kitamaduni ndani ya Taliban, ikiwakilisha maoni ya kwanza juu ya uongozi.

Hayo yakijiri mazungumzo yanaonekana kuendelea baina ya Taliban na maofisa kadhaa wa serikali ya Afghanistan, akiwamo rais wa zamani, Hamid Karzai na Abdullah Abdullah, ambaye wakati mmoja aliwahi kuongoza baraza la majadiliano.

Ofisa mmoja ambaye anafahamu moja kwa moja juu ya mazungumzo hayo, aliyezungumza kwa sharti la kutotajwa jina, alisema kiongozi wa Taliban Amir Khan Muftaqi amewasili mjini Kabul akitokea Qatar.

Muftaqi ni waziri wa zamani wa elimu wakati wa utawala wa mwisho wa Taliban na alianza kufanya mazungumzo na viongozi wa kisiasa wa Afghanistan, hata kabla ya Rais Ashraf Ghani aikimbie nchi. **DW**

MECHI KALI
HOME
AWAY
BIRMINGHAM
3.06 | 3.11 | 2.35
BOURNEMOUTH
1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 433



# LUKAKU AJIMWAGIA SIFA KUTUA CHELSEA

**LONDON,** England

MCHEZAJI aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi, Romelu Lukaku amesema amerudi Chelsea kama "mchezaji aliyekamilika zaidi."

Chelsea ilitumia pauni milioni 97.5 kumsajili mshambuliaji huyo, ambaye awali alijiunga na klabu hiyo akiwa na umri wa miaka 18, akitokea Anderlecht mwaka 2011, kutoka Inter.

Lukaku pia alicheza West Brom, Everton na Manchester United kabla ya kuonyesha kiwango cha kuvutia Inter akifunga mabao 24 kwenye Serie A msimu uliopita kuiwezesha kutwaa taji la kwanza kwa kipindi cha miaka 11.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alitumia misimu miwili kule Serie A, akifunga jumla ya mabao 64 katika mashindano yote baada ya kuwa nguzo muhimu kwa kocha Antonio Conte.

"Najihisi ni mchezaji niliyekamilika zaidi," alisema Lukaku akiiambia tovuti ya klabu hiyo Jumatatu wakati alipoulizwa kulinganisha kati ya ujio wake hapo Stamford Bridge kwa mara ya pili.

"Nimejaribu kupambana sehemu nyingi, lakini sasa najiona ni mchezaji niliyekamilika zaidi na naamini nitakuwa na wakati bora zaidi hapa.

"Si kwamba ni mchezaji mpya, nimekuja sehemu ambayo nilikuwapo na nilikwenda sehemu nyingine kwa ajili ya kukamilika.



# Manahodha Barca kukatwa mshahara

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa Barcelona, Gerard Pique, amesisitiza kuwa manahodha wote wanne wa klabu hiyo watapunguziwa mishahara yao.

Barcelona tayari imethibitisha kwamba, mshahara wa Pique umepunguzwa sana, na ndio iliwezesha kuwasajili Memphis Depay, Eric Garcia na Rey Manaj.

Pique amesisitiza kwamba, manahodha wenzake Sergio Busquets, Sergi Roberto na Jordi Alba, watafuata kutokana na hali mbaya ya kifedha ya Barcelona.

Akizungumza na Movistar baada ya ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Real Sociedad katika mechi ya kwanza ya msimu, Pique alisema: "Kupunguzwa mshahara ndio kitu kilibidi nikifanye, nadhani.

"Nataka kusisitiza kwamba, tumekuwa tukiwasiliana na manahodha wengine juu ya kupunguzwa kwa mshahara na najua watachukua hatua hiyo hiyo hivi karibuni, ni suala la muda tu."Wakati mwingine kuna kutokuelewana," alisema Pique.

"Nimekuwa nikiwasiliana na Sergi, Busi na Jordi, na sote tumewekwa sawa, kujaribu kufikia makubaliano."

## HABARI MICHEZO

# 3,401,140 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/08/21 | 17:00 | Crystal Palace vs Brentford | 2.70 | 3.10 | 2.75 |
| 02. 21/08/21 | 17:00 | Leeds vs Everton | 2.22 | 3.53 | 3.12 |
| 03. 21/08/21 | 17:00 | Coventry vs Reading | 2.20 | 3.25 | 3.20 |
| 04. 21/08/21 | 17:00 | Cardiff vs Millwall | 2.24 | 3.21 | 3.16 |
| 05. 21/08/21 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.76 | 3.25 | 2.47 |
| 06. 21/08/21 | 18:00 | Alaves vs Mallorca | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 07. 21/08/21 | 19:30 | Verona vs Sassuolo | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 21/08/21 | 20:30 | Granada vs Valencia | 2.49 | 3.28 | 2.87 |
| 09. 22/08/21 | 16:00 | Wolverhampton vs Tottenham | 3.42 | 3.22 | 2.21 |
| 10. 22/08/21 | 16:00 | Lokomotiv Moscow vs FC Krasnodar | 2.40 | 3.36 | 2.77 |
| 11. 22/08/21 | 16:00 | Bordeaux vs Angers | 2.80 | 3.30 | 2.48 |
| 12. 22/08/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Malaga | 2.73 | 2.78 | 2.87 |
| 13. 22/08/21 | 21:45 | Nice vs Marseille | 2.88 | 3.18 | 2.48 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 18 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2372 | Kashima Antlers vs V Varen Nagasaki | 1.64 | 3.78 | 4.55 |
| 13:00 | 2652 | Incheon Utd vs Seongnam Ilhwa | 2.57 | 2.91 | 2.76 |
| 13:00 | 4061 | Kawasaki Frontale vs Shimizu S Pulse | 1.46 | 4.24 | 5.79 |
| 13:00 | 4941 | Verspah Oita vs Jubilo Iwata | 5.61 | 4.07 | 1.49 |
| 13:00 | 4943 | Seoul E Land vs Anyang | 2.71 | 3.24 | 2.39 |
| 13:30 | 3701 | FC Seoul vs Jeju Utd | 2.83 | 3.02 | 2.44 |
| 15:00 | 3700 | Brattvag vs Moss | 1.38 | 5.03 | 5.80 |
| 17:00 | 2341 | Kvik Halden vs Senja FK | 1.19 | 6.60 | 9.51 |
| 17:00 | 4256 | Levanger vs Fram Larvik | 1.56 | 4.25 | 4.54 |
| 17:00 | 4541 | Oeygarden FK vs Nardo | 1.59 | 4.26 | 4.35 |
| 17:30 | 2562 | Sotra SK vs Notodden | 2.81 | 3.68 | 2.14 |
| 18:00 | 5645 | Floro vs Baerum | 2.26 | 3.69 | 2.62 |
| 18:30 | 1693 | IF Gnistan vs PK-35 | 2.76 | 3.44 | 2.26 |
| 18:30 | 2956 | Klubi 04 vs VPS Vaasa | 2.90 | 3.43 | 2.18 |
| 18:30 | 3809 | Salpa Salo vs Kaapo Kaarina | 2.38 | 3.52 | 2.56 |
| 19:00 | 1307 | Jerv vs Ham-Kam | 2.52 | 3.53 | 2.41 |
| 19:00 | 1641 | Aasane Fotball vs Grorud IL | 2.08 | 3.68 | 2.91 |
| 19:00 | 2016 | Lyngby vs Fremad Amager | 1.20 | 6.21 | 9.71 |
| 19:00 | 2055 | Sogndal vs Kfum Oslo | 1.70 | 3.73 | 4.16 |
| 19:00 | 2390 | Stjordals-Blink vs Raufoss | 2.72 | 3.69 | 2.19 |
| 19:00 | 3035 | Jammerbugt FC vs Hobro | 2.37 | 3.35 | 2.67 |
| 19:00 | 3725 | Sandnes Ulf vs Strommen | 1.88 | 3.53 | 3.58 |
| 19:00 | 5770 | Aalesunds vs Ranheim | 1.80 | 3.72 | 3.72 |
| 19:30 | 1686 | JSM Skikda vs MC Magra | 8.50 | 4.63 | 1.31 |
| 19:30 | 2311 | WA Tlemcen vs JS Saoura | 2.50 | 3.10 | 2.95 |
| 19:30 | 4836 | FC Ingulets vs Dynamo Kiev | 20.28 | 7.73 | 1.09 |
| 20:00 | 2588 | US Quevilly Rouen vs Bastia | 2.77 | 3.16 | 2.52 |
| 20:00 | 2612 | Ghazl EL Mahallah vs El Entag El Harby | 2.71 | 2.96 | 2.71 |
| 20:00 | 4725 | Floya vs Alta IF | 6.59 | 5.43 | 1.32 |
| 20:00 | 5539 | FC Helsingor vs HB Koge | 1.80 | 3.55 | 3.89 |
| 20:00 | 5900 | Kjelsaas vs Arendal | 2.75 | 3.62 | 2.20 |
| 21:00 | 1433 | Fredrikstad vs IK Start | 2.25 | 3.48 | 2.75 |
| 21:00 | 1518 | Deportivo Espanol vs Excursionistas | 2.66 | 2.76 | 2.81 |
| 21:00 | 4666 | Dudelange vs Wiltz | 1.54 | 4.17 | 4.85 |
| 21:00 | 4988 | Sport Huancayo vs Ayacucho | 2.73 | 2.58 | 2.93 |
| 21:30 | 4264 | Arka Gdynia vs Widzew Lodz | 2.07 | 3.20 | 3.35 |
| 21:45 | 1133 | Nottingham vs Blackburn | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 21:45 | 1821 | Celtic vs AZ Alkmaar | 2.11 | 3.66 | 3.21 |
| 21:45 | 3979 | Birmingham vs Bournemouth | 3.06 | 3.11 | 2.35 |
| 21:45 | 5179 | Middlesbrough vs QPR | 2.38 | 3.10 | 3.00 |
| 21:45 | 5512 | Hull City vs Derby | 1.90 | 3.44 | 3.88 |
| 22:00 | 1733 | BSC Young Boys vs Ferencvaros TC | 1.56 | 3.99 | 5.99 |
| 22:00 | 2037 | The Strongest vs Nacional Potosi | 1.27 | 6.00 | 9.60 |
| 22:00 | 2288 | West Bromwich vs Sheffield Utd | 2.03 | 3.30 | 3.59 |
| 22:00 | 2522 | Misr Lel Makasa vs National Bank | 3.00 | 3.00 | 2.44 |
| 22:00 | 3654 | Benfica vs PSV Eindhoven | 2.12 | 3.50 | 3.30 |
| 22:00 | 4962 | Malmo vs Ludogorets Razgrad | 1.92 | 3.40 | 4.10 |
| 23:00 | 2972 | USM Bel Abbes vs Ol. Medea | 2.00 | 3.25 | 3.95 |
| 23:00 | 4887 | JS Kabylie vs ES Setif | 2.32 | 3.24 | 2.81 |
| 23:15 | 2057 | Deportivo Municipal vs Sport Boys Association | 2.87 | 3.21 | 2.30 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# COURTOIS AJIFUNGA ZAIDI REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

GOLIKIPA wa Thibaut Courtois amekubali kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na Real Madrid.

Madrid wameruhusu mabeki wenye uzoefu Sergio Ramos na Raphael Varane kuondoka klabuni hapo kutokana na kutaka kupunguza tatizo la kifedha lililoongezwa na janga la virusi vya corona.

Lakini, Madrid wameamua kupata mustakabali wa muda mrefu wa kipa Courtois, ambaye amesaini mkataba mpya zaidi.

Courtois alijiunga na Madrid akitokea Chelsea mwaka 2018, baada ya kufanya vizuri na Ubelgiji kwenye Kombe la Dunia huko Urusi ambapo alishinda tuzo ya Golden Glove (Kipa Bora).

Ameendelea kujitambulisha kama namba moja wa 'Los Blancos' baada ya mwanzo mgumu mwanzoni mwa msimu wa pili huko LaLiga na Courtois akiwa amechezea Atletico Madrid kwa mkopo kutoka Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ameisaidia Madrid kutwaa mataji matatu, kushinda LaLiga mwaka 2019-20, Supercopa de Espana msimu huo na Kombe la Dunia la Klabu ya FIFA mwaka 2018.



# *Liverpool, Madrid vitani kwa Mbappe*

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool inatarajia kutunishiana misuli na Real Madrid kupata saini ya mshambuliaji wa Ufaransa na PSG, Kylian Mbappe katika majira yajayo ya kipindi cha joto.

Real Madrid chini ya rais wa klabu hiyo, Florentino Perez, wameweka wazi nia yao ya kutaka kuwasilisha kiasi cha Euro milioni 120, lakini Liverpool wanataka kuingilia kati dili hilo.

PSG wamegoma kumuuza mchezaji huyo huku akiwa amebakiwa na mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa unaotarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mbappe alikutana na rais wa PSG Jumapili kuzungumzia mustakabali wake ndani ya klabu hiyo na hakuhudhulia siku ya kuzaliwa ya mchezaji mwenzake, Ande Herrera.

Hii ni wiki muhimu katika sakata la uhamisho wa Mbappe na mvutano juu ya hatma ya nyota huyo wa Ufaransa umekuwa mkubwa zaidi kuliko hapo awali.

Mbappe tayari ameweka wazi kwa Paris Saint-Germain kwamba, hana mpango wa kuongeza mkataba wake, na klabu yake inajua kuwa kumbakisha msimu huu kutamfanya aondoke kwa uhamisho wa bure msimu ujao.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MARTIAL ATABIRI MAKUBWA KWA VARANE MAN UNITED

Ana uzoefu wa kutosha na ameshashinda vitu vingi akiwa kule Real Madrid na pia...

**MANCHESTER,** England

RAPHAEL Varane ni "mchezaji mkubwa" ambaye haraka atathibitisha thamani yake ndani ya Manchester United, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake, Anthony Martial.

**Wawili hao wamekuwa pamoja mara nyingi kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa na sasa wamejiunga pamoja pale United baada ya Varane kuhamia hapo kutoka Real Madrid.**

Mlinzi wa kati wa Varane alitua hapo kwa ada ya pauni milioni 42.7 na Martial anatarajia mchezaji huyo kuanza maisha hapo Old Trafford, akiwa tayari ameshinda Kombe la Dunia na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Varane, najua tayari bila shaka," alisema Martial, ambaye pia alionyesha kuvutiwa na ujio wa Jadon Sancho, akiiambia tovuti ya United.

"Na akili aliyonayo, najua atasaidia timu yetu kwani ana uzoefu wa kutosha, hivyo wote tunamtarajia hapa.

"Varane ni mchezaji mkubwa. Sifikirii kama atahitaji muda zaidi wa kuzoea maisha ya soka hapa, lakini naamini atakuwa fiti muda si mrefu.

"Ana uzoefu wa kutosha. Yeye ni mchezaji ambaye ameshashinda vitu vingi akiwa kule Real Madrid pia kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa.

"Hivyo, nina uhakika kwamba ataogeza nguvu hapa, kwa sababu yeye ni mchezaji mkubwa na anajua namna ya kuisaidia Man United."

Akiwa amehamia Santiago Bernabeu mwaka 2011, Varane ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne.

Amecheza jumla ya mechi 350 kwa 'Los Blancos' hao na ujio wake Old Trafford utakwenda kuimarisha safu ya ulinzi ya kikosi hicho.

Varane amecheza mechi 79 kwa Ufaransa, akishinda Kombe la Dunia mwaka 2018, kabla ya kucheza mechi zote nne za 'Les Bleus' hao kwenye michuano ya Euro 2020.

## ZISIKUPITE

### PSG YATOA OFA KWA POGBA

KLABU ya Paris St-Germain itatoa ofa kwa kiungo wa kati wa Manchester United raia wa Ufaransa, Paul Pogba, 28 na makubaliano ya mshahara wa pauni 510,000 kwa wiki kama hatua ya kujaribu kumshawishi nyota huyo. ***(Independent)***

### AUBAMEYANG KUONDOKA

ARSENAL huenda ikakubali kumuuza Pierre-Emerick Aubameyang, 31, kwa sababu mchezaji huyo haelewani na kocha, Mikel Arteta. ***(talkSPORT)***

### CITY KWA 'NGONGOTI' WA EPL

MANCHESTER City ni miongoni mwa klabu zinazomnyatia mchezaji mrefu zaidi wa Uingereza mwenye futi 6 na nchi 9 wa Solihull Moors, Kyle Hudlin, 21. Middlesbrough na Cardiff City pia nazo zilikuwa zinamfuatilia. ***(The Athletic)***

### CHELSEA YAMTAKA BELLINGHAM

CHELSEA inawania kumsajili mchezaji wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, 18, kama mbadala wa mchezaji mwenzake wa timu ya England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22. ***(Eurosport, via Sun)***

### HENDERSON NA MKATABA MPYA

MCHEZAJI wa Liverpool na England, Jordan Henderson, 31, amefikia makubaliano ya mkataba mpya wa muda mrefu na klabu hiyo. ***(The Athletic)***

### LAPORTA AMTAJA NEYMAR

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amesema kushindwa kwa watangulizi wake kuwekeza tena pauni milioni 200 kutoka kwa Neymar mwaka 2017, wakati anajiunga na PSG kumechangia mgogoro wa kifedha unaoikumba klabu hiyo. ***(Times)***

### UNITED NA RONALDO JUVE

MANCHESTER United wamearifiwa juu ya mpango ambao huenda unaendelea, kwamba Juventus na Cristiano Ronaldo, 36, wanasemekana wanashughulikia dili la kuondoka kwa mshambuliaji huyo wa Ureno. ***(La Repubblica)***

### ODEGAARD KUREJEA ARSENAL

NYOTA wa Real Madrid, Martin Odegaard, 22, huenda anakaribia kurejea Arsenal, baada ya wakala wa raia huyo wa Norway kwenda London kufanya mazungumzo ya makubaliano ya mkopo wa muda mrefu. ***(Mirror)***

### CITY YAKOMAA NA KANE

MANCHESTESTER City inaendelea na juhudi za kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane, 28, kutoka Tottenham, licha ya Spurs kusema mara kadhaa kwamba haiko tayari kumuuza. ***(ESPN)***

### DIALLO AWANIWA SHEFFIELD

WINGA wa Manchester United raia wa Ivory Coast, Amad Diallo, 19, anahitajika kwa mkopo na klabu ya Sheffield United. ***(talkSPORT)***

HABARI MICHEZO

# HABABUU AAHIDI MAKUBWA SIMBA QUEENS MICHUANO CAF

Na Saada Akida

KOCHA mpya wa Simba Queens, Hababuu Ali, amesema mikakati yake mikubwa ni kuifanya timu hiyo kufuata nyayo za kaka zao na kuwa tishio, kama zilivyo timu kubwa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Simba Queens inatarajia kwenda nchini Kenya kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa Wanawake Kanda ya Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Hababuu alisema anatambua soka la wanawake limekuwa na Simba Queens inatarajiwa kufanya makubwa, hivyo mipango yake ni kukiandaa kikosi hicho vizuri, ili kuwa tishio.

Alisema kazi kubwa anayoifanya ni kutengeneza timu hiyo kwenda kuonyesha ukubwa wake Kenya katika michuano ya Ukanda wa CECAFA na kuwa moja ya timu zitakazopata nafasi kutoka makundi matatu kwenda Misri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kuna mambo makubwa nayaona hapo mbele kulingana na maandalizi tunayoyafanya, tumepata mechi mbili zimenisaidia kuona mapungufu yetu na kufanyia kazi, malengo yangu ni kuwa timu mojawapo kutoka katika makundi ya CECAFA itakayoenda nchini Misri," alisema Hababuu.

Alisema anahitaji kuona timu yake hiyo inafuata nyayo za kaka zao kwa kuvuka katika hatua ya michuano ya CECAFA na kwenda kuliwakilisha vema taifa katika Ligi ya Mabingwa Afrika nchini Misri.

"Simba ni Simba hata kama ni timu ya wanawake, tutambue ni 'Wekundu wa Msimbazi' ambao mashabiki na viongozi wanatarajia makubwa kutoka katika timu zao ikiwamo hii ya wanawake. Kazi iliyopo mbele yangu ni kuvuka nchini Kenya na kuipeleka timu Misri," alisema Hababuu.

Alisema kulingana na maandalizi ya timu yao, wamejipanga vizuri na tayari wameanza kuwafuatilia wapinzani wao waliopangwa kundi moja katika michuano hiyo ya Kenya.

Katika michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Agosti 28, mwaka huu, Simba Queens imepangwa Kundi A pamoja na Lady Doves WFC ya Uganda na PVP FC ya Burundi.

NAJIWEKA FITI...




Beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', akijifua katika mazoezi ya timu hiyo nchini Morocco kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Bara na michuano ya kimataifa. **PICHA: SIMBA**

# *Biashara United yamkamilishia Odhiambo*

Na Saada Akida

UONGOZI wa Biashara United, umesema baada ya kukamilisha usajili wa wachezaji wapya kwa asilimia 90, sasa kazi kubwa wamemwachia Kocha Mkuu, Patrick Odhiambo, kuelekea michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF).

Biashara United na Azam FC zitaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo inatarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa timu hiyo, Selemani Mataso, alisema upande wao wamemaliza masuala ya usajili kulingana na mapendekezo ya kocha Odhiambo, hivyo kazi sasa imebaki kwake kuhakikisha wanaenda kufanya vizuri michuano ya CAF na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema mbali na usajili waliofanya kwa sasa wanaumiza kichwa kuangalia nchi ambayo wataenda kuweka kambi na kupata mechi mbili za kirafiki za ushindani, ili kuwaimarisha wachezaji kimchezo.

"Mipango yetu ya kwanza ni kwenda nchini Kenya, bado hatujafikia muafaka kwa sababu tumepewa taarifa kwamba kulingana na changamoto ya COVID-19, inakuwa vigumu kuchagua moja kwa moja [kwenda huko] hivyo kuachia maamuzi hayo kwa kocha kwenda huko ama kutazama sehemu nzuri ya maandalizi.

"Tayari tumeanza kuwafuatilia wapinzani wetu, tunatambua wenzetu ni wakongwe na wanauzoefu mkubwa wa hii michuano, lakini haitatusumbua kwa sababu Kocha Odhiambo ni mzoefu nayo," alisema Mataso.

Alisema kutokuwa na uzoefu katika michuano hiyo, haiwezi kuwaogopesha na kwamba kikubwa ni kuhakikisha wanapambana kila mechi lengo likiwa ni kutetea nafasi nne ilizonazo Tanzania katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Biashara United ni miongoni mwa timu nne za Tanzania zinazoenda kuwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa na inatarajiwa kucheza mechi ya kwanza dhidi ya FC DIKHIL ya Djibouti.

Timu nyingine ni Simba na Yanga, ambazo zitaiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa barani Afrika.

## KMKM hesabu sasa michuano ya CAF

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM, Ame Msimu, amesema baada ya kushika nafasi ya tatu katika mashindano ya Kombe la Kagame (Cecafa Cup), kwa sasa wanajikita katika maandalizi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Katika michuano hiyo, KMKM itaanzia nyumbani dhidi ya Al-Ittihad ya Libya, mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Amaan kati ya Septemba 10-12, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msimu alisema wanatarajia kuanza mazoezi kuelekea michuano hiyo ya kimataifa mwishoni mwa wiki hii.

"Tumeshaanza kuwafuatilia kwa karibu wapinzani wetu, ili kuona tunajiandaa vizuri, tuna uzoefu katika michuano hii, kwetu sisi ni migumu kwa kuwa tunakutana na timu zinazocheza ligi mbalimbali ambazo nyingine zina viwango vikubwa na wachezaji wazuri, hivyo ili tusonge mbele lazima tuwe na maandalizi mazuri," alisema.

## Ruvu Shooting kuanza kambi leo

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Ruvu Shooting inatarajia kuanza mazoezi leo na kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire, amesema maandalizi yote ya mazoezi na kambi, yameshafanywa na viongozi wa klabu hiyo, ikiwamo usajili wa wachezaji wa zamani ambao mikataba yao imekwisha, lakini wameonekana bado wana umuhimu, pia kusajili nyota wapya.

"Tunaendelea na usajili na kwa kiasi kikubwa tumefanikisha, kilichobaki ni vitu vichache na Jumatano (leo) tutaanza mazoezi na kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu," alisema Ofisa Habari huyo mwenye maneno mengi.

Alisema lengo la kwanza la klabu hiyo ni kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, na malengo mengine yatafuata baadaye kutokana na mazingira na matokeo ya mechi zitakazochezwa.

"Naona kama watu watanishangaa, lakini sisi lengo la kwanza ni kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, tumefanya usajili mzuri. Wachezaji wazuri na tutaendeleza falsafa yetu ya kandanda la kuvutia, lakini safari hii pamoja na ushindi mfululizo," alisema.



Lukaku ajimwagia sifa kutua Chelsea UKURASA 20

# JOTO KALI LAITIBULIA YANGA SC MOROCCO

## ●●● Nabi alazimika kubadili programu ya mazoezi, Aucho, Bangala wawasili, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana Yanga ikianza rasmi kujifua huko Casablanca nchini Morocco ilipoweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika, joto kali walilokumbana nalo jijini humo limetibua programu ya mazoezi ya timu hiyo, hivyo kumlazimu Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, kupangua ratiba yake.

**Yanga ambayo inatarajia kuikaribisha Rivers United ya Nigeria kati ya Septemba 10 -12, mwaka huu, kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imetua juzi nchini Morocco na jana asubuhi ikaanza mazoezi, ambayo walilazimika kuyamaliza mapema kutokana na joto kali.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, ambaye hata hivyo hakusafiri na timu, alisema amepokea taarifa kutoka kwa kocha mkuu kwamba hali ya joto kali katika mji huo imesababisha kubadili programu yao ya mazoezi.

Alisema awali programu ya mazoezi ya timu hiyo ilikuwa kufanya mazoezi mara mbili kwa siku, lakini jana walilazimika kufanya mara moja na kumalizika mapema zaidi kutokana na joto kali.

"Kocha amesema jana wamefanya mazoezi asubuhi kwa muda mchache kutokana na joto kali, hivyo kuanzia kesho [leo], watalazimika kufanya mazoezi mapema sana asubuhi kabla ya jua kuchomoza na kisha hali ikiruhusu baada ya jua kuzama jioni," alisema Bumbuli.

Hali ya jijini Casablanca ilipo kambi ya Yanga kwa sasa inaelezwa ni joto kali tofauti na kambi ya Simba ilipo jijini Rabat nchini humo, ambayo haitofautiani sana na Dar es Salaam kwa sasa.

Kuhusu wachezaji ambao walikuwa hawajajiunga na kikosi hicho, Bumbuli alisema ni wawili tu ambao ni Khalid Aucho na Yannick Bangala Litombo, ambao walitarajiwa kuwasili Morocco jana.

"Wachezaji wote 29 waliopo na timu ya Morocco, wanaendelea vizuri, ila kuhusu Bangala na Aucho na wenyewe walitarajia kujiunga na wenzao leo [jana].

"Bangala ni mchezaji wetu mpya kutoka DR Congo, ambaye utambulisho wake utafanyika nchini Morocco atakapojiunga na wenzake kambini," alisema.

Kutua kwa Bangala, kunaifanya Yanga msimu huu kusajili wachezaji watano raia wa DR Congo ambao wanafanya jumla kuwa sita pamoja na Mukoko Tonombe aliyesajiliwa msimu uliopita. Wachezaji wengine kutoka DR Congo ambao tayari usajili wao wameshautangaza msimu huu ni Fiston Mayele, Djuma Shaban, Jesus Moloko na Heritier Makambo.

Nyota wengine wa kimataifa waliosajiliwa na Yanga msimu huu nje ya DR Congo ni kipa Djigui Diara raia wa Mali na kiungo Mganda Khalid Aucho.



Yusuph Athumani ndani ya uzi mpya wa Yanga nchini Morocco. **PICHA: YANGA**

## Dancan Nyoni, Ndemla waanzishiwa gym Rabat

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Simba kambini jijini Rabat, Morocco sasa limekamilika baada ya nyota wawili waliokuwa hawajaripoti, viungo Dancan Nyoni na Hamisi Ndemla kuwasili juzi na jana kuanzishiwa gym kujiweka fiti.

Simba ilianza mazoezi tangu wiki iliyopita bila wachezaji hao ambao juzi walisafiri katika ndege moja na kikosi cha Yanga kilichoweka kambi jijini Casablanca nchini humo, timu zote zikijiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba itaanzia raundi ya kwanza ya michuano hiyo, wakati Yanga ikianzia nyumbani katika hatua ya awali ya michuano hiyo, ikitarajiwa kuikaribisha Rivers United ya Nigeria kati ya Septemba 10-12, mwaka huu.

Hata hivyo, Simba ambayo itashuka dimbani katika michuano hiyo kuanzia Oktoba 17, mwaka huu, pia itakabiliwa na mechi ngumu dhidi ya Yanga kwenye Ngao ya Jamii mahususi kwa ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu 2021/22 itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Septemba 25 ikiwa ni siku nne kabla ya ligi hiyo kuanza.

Nyoni sasa anaungana na raia mwenzake kutoka Malawi, Peter Banda ambaye naye amesajiliwa msimu huu, lakini alitangulia na kikosi hicho nchini Morocco.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, ameeleza kufurahishwa na na kambi ya timu hiyo jijini Rabat, baada ya kuweka wazi kuwa ni mazingira tulivu na hali ya hewa inamruhusu kukiandaa kikosi chake vizuri.

9 770856 541002 >